# MATUMIZI YA TASHBIHA, SITIARI NA TAASHIRA KATIKA DAMU *NYEUSI NA HADITHI NYINGINE*

**Na**

**LONYCE WAKESHO MWAKIO**

**C50/72309/2014**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

University of NAIROBI Library
0415262 5

**OKTOBA 2016**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine chochote kile.

Jina: **Lonyce Wakesho Mwakio**

Sahihi:..........................................

Tarehe: 10/11/2016

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa kwa utahini kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Jina: **Dkt. Ayub Mukhwana**

Sahihi:..........................................

Tarehe: 10/11/2016

## TABARUKU

Kwa wazazi wangu : Damaris Kijala na Frumence Mwakio walionizaa, wakanitunza na kunipigania kwa hali na mali nipate elimu. Ahsanteni. Kwa mume wangu, Alfred Nyakangi, kwa moyo wa stahamala, utuvu na mahaba. Mola akuzidishie. Kwa wanangu: Esther, Damaris, Michelle na Adrian kwa subira nilipowaacha mliponihitaji zaidi. Mlinipa ari ya kusoma.

## SHUKRANI

Sina budi kuwashukuru wote walionishika mkono katika kufanikisha utafiti huu. Shukrani zangu zisizo kipimo ni kwa Mwenyezi Mungu aliye chanzo cha maarifa kwa kuniwezesha kutimiza utafiti huu. Nawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu Dkt. Ayub Mukhwana na Dkt. J. Michira kwa ushauri wao katika uandishi wa tasnifu hii. Mola awabariki.

Natoa shukrani za dhati kwa wahadhiri wa idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika ambao wamekuwa msingi wa maarifa katika kazi hii. Hawa ni: Prof. Iribemwangi, Prof. Habwe, Prof. Rayya Timmamy, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mwenda Mbatiah, Dkt. Mukhwana, Dkt. Michira, Dkt. Amir Swaleh, Dkt. Jerono, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri na Dkt. Mbuthia. Kwenu Mungu awazidishie hekima na maarifa.

Aidha, nawashukuru wanafunzi wenzangu tulioabiri dau la masomo pamoja hadi ufuoni. Nao ni : Virginia Wairimu, Sarah Mueni, Edward Lokidor, Maurice Lavaya, Jackline Gwako, Seraphine Orucho na Eunice Alivitsa. Mlinipa mawaidha na kunifaa katika mijadala. Mola awajalie mema maishani.

Sitawasahau wazazi wangu, Damaris Kijala na Frumence Mwakio kwa kunielekeza na kunifaa kwa hali na mali ili nipate ufanisi maishani. Mola awape radhi zake. Kwa mume wangu Alfred Nyakangi, subira na welewa wako haumithiliki. Kwa wanangu : Esther Nyamoita, Damaris Kijala, Michelle Kwamboka na Adrian Otwere, mmenipa changamoto ya kusoma. Mmenivumilia. Radhi za Jalali ziwe nanyi dawamu.

## IKISIRI

Katika tasnifu hii tumeonyesha matumizi ya tashbiha, sitiari na tashbiha katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* ambayo ni mojawapo ya hadithi fupi za Kiswahili iliyo na hadithi kumi na tatu zilizoandikwa na waandishi mbalimbali. Katika utafiti huu, mchango wa tamathali hizi za usemi ulichunguzwa katika kuwasilisha dhamira na maudhui ya waandishi wa hadithi zilizo katika diwani hii. Ni hadithi saba kati ya kumi na tatu tulizozishughulikia ambazo tulizichagua kwa kutumia sampuli ya kusudi. Utafiti uliofanywa umekuwa wa maktabani ambapo data iliyokusanywa ilikuwa data isiyo msingi kwani tulitegemea habari zilizohifadhiwa kwenye maandishi mbalimbali. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa, waandishi wa hadithi katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* walitumia mbinu za tashbiha, istiari na taashira kwa utoshelevu na kwa njia mwafaka ili kufikia hadhira yao teule kwa njia ya kisanaa. Utafiti huu umeleta uelewa zaidi wa matumizi ya tamathali hizi kwa kazi husika.

**YALIYOMO**

IKIRARI........................................................................................ii

TABARUKU....................................................................................iii

SHUKRANI.....................................................................................iv

IKISIRI.........................................................................................vii

YALIYOMO....................................................................................viii

**SURA YA KWANZA.......................................................................1**

1.0 USULI WA MADA.........................................................................1

1.1 Tatizo la Utafiti............................................................................1

1.2 Madhumuni ya Utafiti....................................................................2

1.3 Maswali ya Utafiti..........................................................................2

1.4 Sababu za Kuchagua Mada...............................................................3

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti................................................................3

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada............................................................4

1.7 Msingi wa Kinadharia......................................................................7

1.8 Njia za Utafiti...............................................................................14

1.9 Hitimisho....................................................................................14

**SURA YA PILI............................................................................15**

2.0 *MISINGI YA KINADHARIA YA TASHBIHA, ISTIARI NA TAASHIRA..............15*

2.1 Utangulizi....................................................................................15

2.2 Dhana ya Tashbiha........................................................................15

2.2.0 Aina za Tashbiha.........................................................................16

2.2.1 Tashbiha Wazi....16
2.2.2 Tashbiha Fiche....17
2.2.3 Tashbiha ya Kiutendi....17
2.3 Istiari....18
2.3.0 Aina za Istiari....19
2.3.1 Istiari Chakavu....19
2.3.2 Istiari kuu....20
2.3.3 Istiari ya Kikaida....20
2.3.4 Istiari Hisimseto....20
2.3.5 Istiari sahili....21
2.3.6 Istiari Radidifu....21
2.3.7 Istiari Mseto....21
2.3.8 Istiari Changamano....21
2.3.9 Istiari ya Dhana....22
2.4 Taashira....22
2.4.0 Aina za Taashira....23
2.4.1Sinekidoki....23
2.4.2Taniaba....23
2.4.3Lakabu....24
2.5 Hitimisho....24

**SURA YA TATU....25**

3.0 Matumizi ya Istiari katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine....25
3.1 Utangulizi....25
3.2 Samaki wa Nchi za Joto....25
3.3 Damu Nyeusi....27
3.4 Gilasi ya Mwisho Makaburini....29
3.5 Kikaza....30
3.6 Maeko....32

3.7 Kanda la Usufi....36
3.8 Tazamana na Mauti....38
3.9 Hitimisho....41

**SURA YA NNE....42**

4.0 Matumizi ya Tashbiha katika Diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine....42
4.1 Utangulizi....42
4.2 Samaki wa Nchi za Joto....42
4.3 Damu Nyeusi....45
4.4 Gilasi Mwisho Makaburini....47
4.5 Maeko....50
4.6 Kanda la Usufi....51
4.7 Tazamana na Mauti....54
4.8 Hitimisho....55

**SURA YA TANO....56**

5.0 Matumizi ya Taashira katika Diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine....56
5.1 Utangulizi....56
5.2 Samaki wa Nchi za Joto....56
5.3 Damu Nyeusi....58
5.4 Gilasi ya Mwisho Makaburini....59
5.5 Kikaza....60
5.6 Maeko....61
5.7 Kanda la Usufi....62
5.8 Tazamana na Mauti....63
5.9 Hitimisho....64

**SURA YA SITA**........................................................................................**65**

6.0 Muhtasari, Mahitimisho na Mapendekezo........................................................65

6.1 Utangulizi.........................................................................................65

6.2 Muhtasari..........................................................................................65

6.3 Mahitimisho......................................................................................66

6.4 Mapendekezo....................................................................................67

MAREJELEO.............................................................................................68

# SURA YA KWANZA

## 1.0 USULI WA MADA

Tashbiha, taashira na istiari ni tamathali za usemi zinazotumiwa na waandishi wa kazi za fasihi ili kutekeleza majukumu mbalimbali. Utanzu mmojawapo wa fasihi unaotumia mbinu hizi ni hadithi fupi. Tamathali hizi za semi huwa na majukumu ya kutekeleza. Kulingana na Wamitila (2008), majukumu ya tamathali hizi za usemi ni pamoja na urembeshaji wa kinachozungumziwa ili kiwe na mvuto mkubwa wa kisanaa, ufafanuaji wa kinachohusishwa na hatimaye kufanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani. Mbinu hizi ni miongoni mwa tamathali za usemi zilizotumika katika mkusanyiko wa hadithi za *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* ili kufafanua, kufanya thabiti na kurembesha kinachorejelewa.

Kwa kuwa lugha ya fasihi ni ya kihisia na inabeba kiimbo na mkabala wa mwandishi, tamathali hizi huchangia pakubwa katika kupanga mawazo ya mwandishi kwa njia ya kuvutia. Mbali na kuwasilisha ujumbe fulani, lugha ya fasihi humshawishi msomaji ili kujaribu kuuathiri na pengine kubadilisha msimamo wake. Kwa hili, hisia za ndani alizo nazo mwandishi huweza kujidhihirisha kupitia tamathali hizi.

Mtindo huhusisha mambo mawili makuu; wazo (maudhui) na jinsi wazo linavyoelezwa (fani). Maudhui huweza kupitishwa kupitia wahusika na jinsi lugha ilivyotumiwa. Tamathali hizi za usemi ni za ulinganisho na kwa hivyo, huleta ulinganifu unaotoa uzito wa lugha yenye mashiko na iliyoteuliwa. Karanja (2014) asema kuwa, hizi tamathali za usemi huleta kufasiriwa kwa uangalifu kwa yale yaliyosemwa.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Katika utafiti huu, tulichunguza jinsi tashbiha, taashira na sitiari zilivyotumika kuwasilisha dhamira katika *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.* Katika usomaji wetu, tuligundua kuwa diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* tuliyoihakiki haijahakikiwa na mtaalamu yeyote hasa kwenye kipengele hiki cha mtindo. Kwa kuchanganua tamathali za semi, tumeliziba pengo hilo na kutoa mchango wetu wa kitaaluma.

Uwasilishaji wa mawazo ya mtunzi wa kazi yoyote ya fasihi huweza kufanikishwa kupitia matumizi ya mbinu mbalimbali za kifasihi. Tashbiha, taashira na istiari ni miongoni mwa tamathali za usemi zilizopewa nafasi muhimu katika jamii nyingi ambapo fasihi kwa jumla hukaririwa au kuandikwa. Tangu enzi za kina Aristotle na Plato, tamathali za semi zimetumika kueleza dhana mbalimbali katika jamii. Aidha, tamathali hizi za usemi hutumika kufumbata ujumbe fulani ili kufikia hadhira teule.

Majukumu ya lugha ya kitamathali ni pamoja na kurembesha kinachozungumziwa au kurejelewa na hiyo lugha. Pia, lugha ya kitamathali huweza kufafanua kinachohusishwa. Aidha, tamathali hizi zina jukumu la kufanya thabiti kinachorejelewa. Tamathali za usemi zinapotumiwa vizuri huvutia hadhira kwa mnato wake. Vilevile, tamathali hizi huweza kuonyesha umahiri wa mwandishi na uasilia wa kazi husika. Isitoshe, tamathali hizi kwa kiwango fulani huonyesha mazingira ya mwandishi. Ni kutokana na hayo yote ambapo tulichagua kuangazia matumizi ya tashbiha, taashira na istiari katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.*

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

a. Kuchanganua tashbiha, taashira na sitiari katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.*

b. Kutathmini mchango wa tamathali hizi za usemi katika kuwasilisha dhamira katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.*

## 1.3 MASWALI YA UTAFITI

a. Je, tashbiha, taashira na sitiari zimetumika katika *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine?*

b. Je, tamathali hizi za usemi zina mchango gani katika kuwasilisha dhamira katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine?*

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Sababu mojawapo ya kuchagua mada hii ni kuwa, katika usomaji wetu wa *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* tumegundua kwamba, nyingi ya hadithi hizi zimetumia tashbiha, taashira na sitiari katika kuwasilisha dhamira.

Aidha, mtindo katika utanzu wa hadithi fupi haujashughulikiwa sana kama katika tanzu nyingine za fasihi andishi ya Kiswahili. Ni kutokana na ugunduzi huu ambapo tulipata msukumo wa kufanya uhakiki wa kimtindo tukiwa na malengo kuwa matokeo ya utafiti huu yatawafaa wasomaji wa hadithi hizi ili wawe na uelewa mpana wa hadithi hizi.

Aidha, watafiti wengine watapata shauku ya kuhakiki hadithi hizi kwa kuzingatia vipengele vingine. Sababu nyingine ni kwamba, tumegundua kuwa diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* tuliyoihakiki ilikuwa haijafanyiwa uhakiki wa kitaaluma na mtaalamu yeyote. Kwa hivyo, utafiti wetu utawafaidi wasomaji na kuchangia pakubwa katika uhakiki wa hadithi fupi za Kiswahili kwa jumla. Vilevile, matokeo ya utafiti huu yatawawezesha watafiti wa baadaye kuhakiki hadithi hizi na nyingine kwa kuzingatia tamathali nyingine za lugha.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Utafiti huu ulijikita katika hadithi saba kati ya kumi na tatu zilizomo katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Utafiti wetu uliegemea pakubwa hadithi hizi kwa sababu ndani yazo mna matumizi ya tashbiha, taashira na sitiari ambazo ni baadhi ya tamathali za usemi zinazotumiwa kuwasilisha dhamira katika kazi za kifasihi. Hadithi hizi ni: *Damu Nyeusi, Samaki wa Nchi za Joto, Gilasi ya Mwisho Makaburini, Kikaza, Maeko, Kanda la Usufi* na *Tazamana na Mauti.*

Waandishi wa hadithi hizi pia wametumia mbinu nyingi za lugha au tamathali za semi katika kazi zao kama vile; chuku, tashihisi, nahau, methali na takriri. Hata hivyo, sisi tulichanganua semi tatu pekee ambazo ni tashbiha, taashira na sitiari kwa sababu zinashabihiana kwani zote ni tamathali za ulinganisho.

## 1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Katika fasihi ya Kiswahili, kunao waandishi/watafiti watangulizi katika uwanja huu wa uchanganuzi wa kimtindo. Ufuatao ni muhtasari wa mada mbalimbali kuhusu tafiti za awali za kimtindo. Kitsao (1975), amehakiki mtindo katika kazi za kinathari za Kiswahili akitumia nadharia ya Crystal na Davy (1969), inayohusisha Kiingereza kinachozungumzwa. Kitsao amefafanua kwa undani dhana ya mtindo na elimumitindo huku akionyesha namna mtindo unavyojitokeza katika kazi alizozishughulikia zikiwemo; mashairi, tamthilia, hadithi fupi na riwaya. Utafiti wetu unahusu uchanganuzi wa vipengele vya mtindo katika hadithi fupi. Kwa hivyo, matokeo ya utafiti wa Kitsao ni muhimu katika utafiti wa mada yetu kwa kuwa yalitupatia mwelekeo wa kuvihakiki vipengele vya mtindo katika hadithi fupi tulizozishughulikia. Hata hivyo, utafiti wetu uliangazia vipengele vitatu pekee vya mtindo ambavyo ni tashbiha, taashira na istiari kinyume na uchanganuzi wa Kitsao ulioangazia mtindo katika ujumla wake na jinsi unavyojitokeza katika kazi za fasihi kwa ujumla.

Olali (2010), amehakiki riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), ambapo utafiti wake ulihusu uchanganuzi wa tamathali za usemi na mbinu za lugha katika riwaya hii. Utafiti huu ulitufaa sana katika uchanganuzi wa kipengele cha mtindo katika hadithi fupi tulizozishughulikia. Tofauti na utafiti wetu ambao ulijikita katika hadithi fupi, utafiti wa Olali ulijikita katika riwaya.

Lugwiri (2011), amechanganua tamathali za usemi zilizotumika katika utenzi wa *Tambuka*. Katika utafiti huu, Lugwiri ametumia nadharia ya umitindo na anabainisha wazi jinsi vipengele vya tamathali za usemi vinavyobainika katika utenzi husika. Anaonyesha kuwa, tamathali za usemi ni mihimili mikuu ya maudhui na dhamira. Kwa kuwa utafiti wetu ulihusu mtindo katika hadithi fupi, matokeo ya utafiti wa Lugwiri yalitufaa kwani ametumia nadharia ya umitindo kama sisi. Hata hivyo, sisi tumeangazia mtindo katika hadithi fupi ilhali yeye aliangazia mtindo katika ushairi.

Karanja (2014), ni mtafiti aliyeshughulikia jinsi istiari, tashbiha na taashira katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* zilivyotumiwa kuwasilisha dhamira. Karanja ametumia nadharia ya uhakiki wa kimtindo kuonyesha jinsi tamathali hizi za usemi zilivyotumiwa na mwandishi kufikia dhamira yake kwa hadhira yake teule. Nadharia hii ilimwezesha kuhakiki viashiria vilivyotumiwa kuunda tamathali za usemi ; istiari, taashira na tashbiha katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* na kuvipa maana viashiria hivi. Vivyo hivyo, utafiti wetu ulitumia umitindo kuhakiki tamathali za semi katika hadithi fupi. Kwa hivyo, utafiti wa Karanja umetufaa pakubwa. Tofauti na utafiti wa sasa uliochunguza hadithi fupi, utafiti wa Karanja ulihusu ushairi.

Murumba (2013), aliangazia jinsi mtindo unavyojitokeza katika riwaya *'Watu wa Gehenna'* ambapo alichambua vipengele mahsusi vya kimtindo vinavyodhihirika katika riwaya hii na kutoa maelezo ya jinsi vinavyoathiri muundo wake na vinavyochangia uwasilishaji wa ujumbe. Matokeo ya utafiti huu yametufaa sana katika kuchanganua vipengele vya kimtindo tulivyovishughulikia. Hata hivyo, upeo wa kazi ya Murumba ni tofauti na hii yetu kwa kuwa alichambua riwaya moja huku nasi tukizichunguza hadithi fupi saba.

Mbuthia, E. (2005), amehakiki kipengele cha mtindo na maudhui kwa kina. Amechanganua diwani kumi na nne za Kiswahili akianza na zile za awali mpaka zile za kisasa. Uhakiki alioufanya wa kimtindo umetufaa katika kazi yetu kwani tumerejelea baadhi ya vipengele vya mtindo alivyovijadili.

Ongarora, S. (2007), aliangazia mtindo katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Katika kazi hii, amechambua matumizi ya methali, semi, tamathali za semi na mbinu nyingine za lugha. Utafiti huu umetufaa kwani tumeangazia matumizi ya tamathali za usemi katika hadithi fupi. Kazi hii ya Ongarora yatofautiana na utafiti wetu hasa kwenye mahusiko ya upeo.

Indagasi, H. (1988), amezungumzia maswala kadhaa ya elimumitindo. Amezungumzia historia ya elimumitindo na viwango vya kuchunguza mtindo kama vile fonolojia, sintaksia, msamiati, semantiki na tamathali za usemi. Uchanganuzi huu umetupatia mwelekeo mzuri wa kuchambua kazi yetu kwa vile tumeshughulikia matumizi ya lugha katika kiwango cha tamathali za usemi.

Leech, G. Na Short, M. (1981), wametalii mawanda ya mtindo. Pia, wamejadili kuhusu nadharia ya elimumitindo. Isitoshe, wameangazia kuhusu uhusiano wa mtindo na maudhui. Mbali na hayo, wameainisha viwango vya kuchanganua mtindo. Ingawa kazi yao imejikita katika tanzu zote za fasihi, mchango wao umetuongoza katika kuchanganua mtindo katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Yaani, kazi za waandishi hawa ni kama mhimili kwa kazi hii ya sasa japo tumetofautiana kwenye upeo na mipaka.

Wales, K. (2001), amefafanua kwa kina dhana ya mtindo na elimumitindo. Aidha, ametoa fafanuzi mwafaka za tamathali anuwai za usemi. Hivyo basi, kazi yake imetufaa katika kurejelea dhana mbalimbali katika utafiti wetu wa mtindo.

Mohamed, S.A. (1995), amefafanua maana ya mtindo na kuangalia dhana mbalimbali za mtindo. Mjadala wake kuhusu mtindo umekuwa wa manufaa kwetu kwa sababu tumechunguza vipengele vya kimtindo katika hadithi fupi.

Mbatiah, M. (2000), amehariri diwani ya *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* na amegusia swala la mtindo katika hadithi fupi. Amefafanua dhana ya mtindo na kuonyesha kuwa mtindo huhusishwa na maudhui. Mchango wake ni muhimu katika kazi yetu kwa vile amejikita katika hadithi fupi. Hata hivyo, yeye amezungumza kinadharia zaidi huku nasi tukitumikiza yale aliyoyasema kimatendo.

Msokile, M. (1992), amejadili vipengele mbalimbali vya fani. Moja kati ya vipengele hivyo ni mtindo. Anaeleza vipengele vya mtindo kuwa ni uchaguzi wa maneno, matumizi ya taswira na ishara, maelezo na masimulizi miongoni mwa mengine. Uchambuzi wake wa mtindo umekuwa msingi mzuri wa kuchambua vipengele vya kimtindo katika kazi yetu.

Mohochi, E. (1995), amechanganua vipengele vinne vya fani katika hadithi nne za waandishi tofauti. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti wetu kwani inaangazia kipengele cha kimtindo ambacho ni lugha na ambacho sisi pia tumeshughulikia.

## 1.7 MSINGI WA KINADHARIA

Nadharia ambayo iliafiki utafiti huu ni ya uhakiki wa mtindo. "Mtindo" hutumiwa kurejelea jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani na kwa lengo fulani (Leech na Short 1981:10). Mwanaisimu wa Kiswisi Ferdinand de Saussure alitofautisha dhana za "Parole" na "Langue" kwa kurejelea lugha. Kulingana na de Saussure, "Langue" ni utaratibu mzima wa kanuni za lugha husika. "Parole" ni matumizi ya utaratibu wa lugha ya mzungumzaji binafsi. "Parole" ni uteuzi wa kanuni ambazo msemaji huzitumia katika uandishi na uzungumzaji wake. Kwa hivyo, mtindo ni kama "Parole" kwa kuwa ni uteuzi kutoka katika utaratibu wa kanuni zilizoko za lugha. Kwa muhtasari, lugha inayojulikana na wazungumzaji "Langue" inaundwa kutokana na kanuni za lugha "Langue" pamoja na matumizi yake katika mazungumzo na maandishi "Parole" (Chapman 1973:9, Kitsao, 1975:8-11, Leech na Short 1981:10-11 na Wales 1990:287).

Mtindo unaweza kuhusishwa na lugha iliyoandikwa, lugha ya kifasihi na isiyokuwa ya kifasihi ingawa kwa kawaida unahusishwa na matini za kifasihi zilizoandikwa. Katika uandishi wa fasihi, mtindo hutumiwa kwa maana nyingi; ni mazoea ya lugha ya mtu binafsi au jamii-lugha. Hii ndiyo maana ambayo huwajia watu akilini wanapozungumza kuhusu mtindo wa kuzungumza au kutoa hotuba hadharani. Mtindo ni upekee wa kujieleza katika maandishi au mazungumzo. Ni jinsi waandishi huandika na pia ni njia tofauti za watu wanavyozungumza au kuandika katika miktadha ya kawaida ya kila siku.

Mwasisi wa nadharia ya umitindo ni Geoffrey Leech ambaye alipokuwa akiandika tasnifu yake ya uzamili, alipenda lugha ya kifasihi, ambayo aliitumia kuandika makala yake mbili, mnamo mwaka 1965 na 1966. Kutokana na kazi hizi za Leech, isimu ya kisasa ilihusishwa na usomaji/ufundishaji wa lugha ya fasihi. Mtazamo huu ulizua ugomvi baina ya wasomi wa fasihi na wa isimu. Ni wakati huu ambapo Leech alionelea mwafaka upatikane baina ya mitazamo-husika miwili; wa kiisimu na ule wa kifasihi. Alifanya hivi kwa kuandika kitabu chake, "*A Linguistic Guide to English Poetry*" (1969), ambamo alishughulikia suala la mtindo katika kuchanganua matini za kifasihi. Leech (1969:2) anasema yafuatayo kuhusu mtindo:

> Elimumitindo ni uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu. Kama taaluma, inafungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu ingawa haijisimamii kivyake. Msamiati mpana wa kimsingi wa uhakiki wa kifasihi hususan sitiari, taswira, kinyume, kinaya, kejeli, usambamba na jazanda hauwezi kufafanuliwa bila kurejelea dhana za kiisimu.

Kwa hivyo, kama msingi wa kutumia taaluma za kifasihi na kiisimu, elimumitindo ni uwanja ambamo masuala haya hushughulikiwa. Akizungumzia lugha katika fasihi, Leech anasema kuwa, athari ya matini yoyote ile huamuliwa kwa kiasi kikubwa na mtindo. Msimamo wake ni kwamba, mtindo ni njia na jinsi lugha inavyotumiwa, nao mtindo haujabanwa tu katika fasihi ila ni sehemu ya usemi wowote ule kwa sababu katika kila muktadha, msemaji huchagua jinsi ya kuzungumza.

Kwa muhtasari, umitindo hutumiwa kurejelea mkabala wa uchanganuzi wa matini za kifasihi kwa kuchunguza mtindo kwa njia ya kisayansi – yenye nidhamu na taratibu za kitaaluma; na huweza kuelezwa kama nadharia iliyo katikati ya isimu na fasihi. Kimsingi, nadharia hii ina mwelekeo wa kifani na inadhamiriwa kuchunguza mtindo wa kinachosemwa (maudhui) na jinsi kinavyosemwa (fani). Nadharia ya elimumitindo imepitia hatua kadhaa kufikia sasa.

Wamitila (2003:39) anasema:

> Dhana hii hutumiwa kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi wa lugha na uchanganuzi wa jinsi mbalimbali za kuelezea matukio katika kazi za kifasihi. Ni taaluma iliyoko kati ya uchanganuzi wa lugha na uchunguzi wa fasihi au jinsi lugha inavyotumiwa katika matini au kazi za kifasihi. Elimumitindo huweza kuhusisha uchunguzi wa sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi fulani na zinazomtambulisha mwandishi anayehusika.

Katika nukuu hii, Wamitilia anaunga mkono madai ya Leech (1969) kwamba, nadharia ya elimumitindo ni mwafaka katika kuhakiki kazi za kiisimu pamoja na za kifasihi. Hii ni kwa sababu elimumitindo huwezesha kuchunguza jinsi lugha ilivyotumiwa katika matini za kifasihi na hivyo basi, kuwezesha uchunguzi wa vipengele vya fani na maudhui. Kwa kuchangia dhana ya umitindo, Crystal na Davy (1969:10) wanasema kuwa;

> Lengo la umitindo ni kuchanganua tabia za lugha kwa madhumuni ya kubainisha sifa mahsusi zinazobanwa katika miktadha maalumu kutoka kwa sifa kijumla za kiisimu ambazo hupatikana katika kila muktadha wa matumizi ya lugha.

Dhana ya umitindo, kulingana na Barry (200:205), iliibuka kutoka nadharia ya balagha ya zamani za kina Aristotle na Cicero katika enzi ya Uyunani na Urumi. Hawa walitathmini jinsi ya kuzungumza, kupanga mjadala, kutoa na kuwasilisha hotuba.

Naye Wamitila (2008) asema kuwa, nadharia ya balagha katika jadi zizi hizi za Kiyunani na Kirumi ilitathmini jinsi ya kuzungumza au kuwasilisha ujumbe kwa njia ya maandishi.Wananadharia Aristotle na Cicero walijihusisha na ufafanuzi wa matumizi ya lugha katika matumizi, uteuzi wa maneno, mpangilio wake na namna ya kuunda ruwaza. Pia, walieleza matumizi ya tamathali za usemi na mbinu nyingine za kilugha ili kuleta athari kubwa.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), wana urasimi wa Kirusi na wana umuundo hushikilia kuwa lugha anayoipata mtu huwa matokeo ya maingiliano ya kijamii ambayo kwa vyovyote vile huwahusisha wazumgumzaji binafsi. Wamitila anaieleza hali ya ishara moja kuwa na maana nyingi kwa kuiweka au kuikita maana kwenye muktadha wa kijamii. Yaani, ishara huwa na athari kubwa juu ya maudhui.

Mwelekeo huu wa mtindo kama asemavyo Wales (2001:437), ulianza kuenezwa Uropa hadi Marekani na watu kama Halliday na kupanuka kutoka ufinyu wake kutumia vipengele vya kisarufi ambavyo ni vya kifonolojia na kisintaksia na ulianza kutumiwa katika aina nyingine za kifasihi kama riwaya na tamthilia.

Baadhi ya mpanuko huu wa miaka ya 1980, Barry (2002) na Simpson (2004), wanaeleza kuwa matokeo yake yalikuwa umitindo mpya. Mwelekeo huu mpya umezingatia mambo ya kimsingi ambayo hushughulikiwa na kuchunguzwa katika kazi zozote za kifasihi panapotumika mwelekeo huu wa uhakiki kimtindo. Wamitilia (2008), aliyaeleza zaidi mambo ya kimsingi ambayo huchunguzwa katika fasihi mhakiki anapotumia nadharia ya elimumitindo;

i. Lugha ya kitamathali na mtindo
ii. Uteuzi na mtindo
iii. Sarufi na mtindo
iv. Usimulizi na mtindo
v. Uchimuzi na mtindo
vi. Itikadi, mtazamo na mtindo
vii. Muwala, mshikamano na mtindo
viii. Mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo

### 1.7.1 Lugha ya kitamathali na mtindo

Wanamitindo wengi wameng'amua kuwa tamathali za usemi zimepewa nafasi kubwa katika mazungumzo ya kila siku, hivi kwamba baadhi ya maana katika lugha nyingi huwa na asili yake kutokana na tamathali hizi. Wamitila (2003) asema ya kwamba katika ushairi aghalabu maana huwa inawasilishwa na mitindo ya kitamathali bali sio ule wa moja kwa moja. Aliainisha haya katika makundi manne makuu ambayo ni: tamathali/rasamu za kisentensi; tamathali/rasamu za tafkira; tamathali za kimaeneo na tamathali za sauti. Wamitila amejumlisha mambo haya ili kuleta mtindo wa uandishi mbali na kuiremba lugha. Kwa hivyo, tamathali kama vile tashbiha, sitiari, taashira, ritifaa na tanakali za sauti huweza kutumiwa na mwandishi ili kuwa na mtindo usio wa moja kwa moja kueleza maana.

### 1.7.2 Uteuzi na mtindo

Simpson (2004) asema kuwa kila mtunzi wa kazi ya fasihi huwa na malighafi kadhaa ya lugha lakini huteua kutumia mojawapo badala ya mengine katika muktadha mahsusi. Uteuzi huu huongozwa na kaida fulani za kiutanzu au mtindo wa kibinafsi wa mwandishi.

Msamiati anaouteua mwandishi pia huweza kuchangiwa na maswala kama mandhari, mbinu za fasihi simulizi, mada na walengwa. Ingawa vipengele hivi huchangia mtindo, huenda mwandishi asitumie vyote bali ateue vichache vinavyoafiki uwasilishaji wake. Kwa kufanya uteuzi huu, mwandishi huwa na lengo la kuleta athari kwa msomaji ili apate ujumbe aliodhamiria mwandishi.

### 1.7.3 Usimulizi na Mtindo

Usimulizi hurejelea hali ya kuwepo kwa matukio katika hadithi yanayosimuliwa na kuleta mabadiliko. Suala hili la uhakiki wa kimtindo huhusika na ploti na msuko wa hadithi. Matukio na visa katika matini ya kifasihi lazima yafuate ruwaza fulani. Msuko huweza kuwa wa moja kwa moja au changamano. Mpangilio wa matukio huenda sambamba na wakati kutoka mwanzo hadi mwisho, au huwepo mpangilio wa matukio kwenda mbele na nyuma (mbinu rejeshi ).

Aidha, kuna utoaji masimulizi. Mara nyingi huwepo sauti inayotoa masimulizi aidha ya mwandishi au ya mhusika mmojawapo. Masimulizi huweza kutolewa katika nafsi ya kwanza au katika nafsi ya tatu au mara nyingine nafsi zote hutumiwa. Kwa hili, mhakiki anaweza kubainisha sifa hizi za kimtindo na athari inayoletwa kwa wanaosimuliwa.

Kimsingi, matini za kifasihi huwa na muundo wenye sehemu tatu; mwanzo ambao ndio unaoelekeza kwenye mfuatano wa kiwakati. Jukumu la mwanzo ni mfichuo wa mhusika au dhamira. Mfichuo huu unaweza kuwa mwanzoni, wa hatua kwa hatua, mfichuo uliokawizwa na mfichuo ulioahirishwa; kisha sehemu ya kati (kiini), na mwisho ambao una utatuzi wa tatizo kuu ambalo ndilo kiini cha mgogoro (Simpson 2004;18 na Wamitila 2008;515-516).

### 1.7.4 Sarufi na Mtindo

Kiwango cha kisarufi ndiyo nguzo ya matamshi ya kiisimu na ni msingi mkuu wa lugha unaodhibiti matamshi ya lugha yenyewe. Sarufi hujumlisha viwango vya kimofolojia na kisintaksia. Hushughulikia mpangilio wa maneno katika sentensi kwa kubainisha visehemu vyake ambavyo huwa na dhima maalum. Ukiushi wa kisarufi huhusisha masuala kama kubananga sarufi, matumizi ya neno moja kuanza kila mstari katika nyimbo na mashairi na kurudiwarudiwa kwa sentensi au kifungu. Huwepo pia, ukiushi wa kilahaja na matumizi ya sajili. Kwa ujumla, sarufi na mtindo huzingatia ukiushi katika muundo wa kawaida wa matumizi ya lugha, urefu wa sentensi (fupi na ndefu) na sentensi zenye dosari (Leech 1969 na Wamitila 2008:512). Kutokana na haya yote, ni vyema mhakiki wa kimtindo ashughulikie mambo haya yote ili aonyeshe athari yake kwa muundo na maana ya kazi ya fasihi au matini yenyewe.

### 1.7.5 Uchimuzi na Mtindo

Uchimuzi ni matumizi ya lugha kwa namna inayofanya kitu kinachozungumziwa kutokea kwa uwazi zaidi. Hujitokeza katika kiwango cha kisintaksia au kisemantiki na ambapo huonyesha jinsi matumizi ya lugha yanavyoathiri maana kwa njia fulani. Uchimuzi mara nyingi huhusisha matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Huwepo matumizi ya tamathali za usemi, mbinu ya kinaya, mbinu ya kweli-kinzani (paradoksi), mbinu ya oksimora (tanakuzi) na mbinu ya sitiari. Pia huhusisha matumizi ya jazanda, yaani lugha ya picha ziwe za kimaelezo au za kiishara ambazo si taswira au picha tu bali zina ujumbe wa ziada (Wamitila 2008:518).

### 1.7.6 Mtazamo, Itikadi na Mtindo

Mwandishi huchukua mkabala fulani kuhusu anayoyazungumzia na mtazamo huu unaweza kuwa na mchango mkubwa kwenye upokezi wa maneno anayoyasema na jinsi mlengwa anavyoyaelewa au kukipokea kisa kinachosimuliwa. Lugha huwa ni nyenzo muhimu ya kubainisha itikadi hiyo. Aidha, mtazamo wa itikadi ya mwandishi huweza kujidhihirisha kupitia uteuzi wa wahusika, mandhari na hata maudhui.

Mchanganuzi wa kimtindo anastahili kuchunguza jinsi uteuzi wa maneno au uteuzi wa kiisimu unavyochangia katika kuangazia itikadi hiyo (Wamitila 2008:519-520).

### 1.7.7 Mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi wa mawazo.

Katika kiwango hiki, mhakiki wa kimtindo huchunguza mazungumuzo na usemezano baina ya wahusika na mbinu nyingine ambazo zinatumiwa katika mazungumzo hayo kwa lengo la kuwasilisha usemi na mazungumzo ya wahusika. Aghalabu, binadamu hutumia lugha kwa njia ambazo zinatofautiana katika viwango vya msamiati, miundo ya sentensi au mkazo. Tofauti hizi za kimatumizi zinapaswa kuonekana katika tungo za kifasihi hususan hadithi fupi. Ni jukumu la mhakiki kuangazia tofauti zilizoko katika matumizi ya lugha miongoni mwa wahusika. Kulingana na Ngara (1982), huku kutofautisha wahusika katika misingi ya matumizi ya lugha ni sifa nzuri ya lugha katika jamii.

### 1.7.8 Muwala na Mshikamano

Hizi ni mbinu mbalimbali za kiisimu ambazo huwezesha maneno ya aya na sentensi, virai na vishazi kuhusiana na kuleta maana iliyonuiwa. Hii huleta umoja na uthabiti. Kama tulivyoona hapo juu, swala la mtindo katika fasihi ni pana na nadharia ya elimumitindo ina viwango vingi vya kuweza kuchanganulia matini za kifasihi. Hata hivyo, katika uhakiki wetu, hatukutumia vigezo vyote ila tuliteua tu baadhi ya vipengele ambavyo vilifaa katika kushughulikia mada yetu na kuvichunguza kwa undani. Kwa kuwa utafiti huu unahusu matini ya kifasihi, tulidhamiria kuchunguza vipengele vya tamathali za usemi ambapo tulichukua vitatu. Navyo ni taashira, istiari na tashbiha ambavyo huwa na nafasi kubwa katika nadharia ya uhakiki wa kielimumitindo.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti wetu umekuwa wa maktabani kwa kuwa ni utafiti wa fasihi andishi. Data tuliyoikusanya ni data isiyo ya msingi kwani tulitegemea habari ambazo zimehifadhiwa kwenye maandishi mbalimbali. Tulisoma kazi mbalimbali zinazoeleza na kutumia tashbiha, istiari na taashira. Vilevile, tulirejelea vitabu, makala na maandishi yanayohusu nadharia ya elimumitindo ambayo ndiyo tuliyotumia katika utafiti wetu. Isitoshe, tumerejelea makala na tasnifu mbalimbali zilizoandikwa kuhusu umitindo katika kazi za kifasihi na pia tumekita utafiti wetu katika tovuti kwenye mitandao ya kiusomi ili kupata yalioandikwa kuhusu nadharia ya elimumitindo.

Tulisoma *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* ili tuweze kueleza msingi wa mbinu hizi tatu kwa ujumla. Njia ya uteuzi wa data yetu imekuwa sampuli ya kusudi ambapo tulisoma hadithi zote katika mkusanyiko huu wa hadithi kisha tukachagua baadhi ya hadithi ambazo zimetumia mbinu za tashbiha, sitiari na taashira.

Hatimaye, tuliichanganua data yetu kwa kubainisha jinsi vipengele tulivyoviangazia (tashbiha, sitiari na taashira) vilivyoendeleza athari fulani katika *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.* Kisha, tumeangazia jinsi mbinu hizi zilivyotumika katika hadithi tulizoteua. Tumeeleza maana ya kila moja ya mbinu hizi na jinsi zilivyotumika katika kuwasilisha dhamira.

## 1.9 HITIMISHO

Katika sura hii tumetoa maelezo mafupi kuhusu mbinu za tashbiha, sitiari na taashira. Tumeangazia pia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti na maswali ya utafiti. Aidha, tumetoa sababu zetu za kuchagua mada tuliyoishughulikia. Tumeonyesha pia upeo na mipaka ya utafiti wetu ambapo kati ya hadithi kumi na tatu zilizomo kwenye diwani hii, ni hadithi saba pekee tulizozishughulikia. Zaidi ya hayo, tumeangazia yaliyoandikwa kuhusu mada tuliyoishughulikia. Isitoshe, tumeshughulikia msingi wa kinadharia uliotuongoza katika utafiti huu ambapo tulitumia uhakiki wa kimtindo. Hatimaye, tumetaja mbinu tulizozitumia katika utafiti wetu.

## SURA YA PILI

## 2.0 MISINGI YA KINADHARIA YA TASHBIHA , ISTIARI NA TAASHIRA

### 2.1 Utangulizi

Sura hii ni ya muhimu sana kwani masuala yatakayojadiliwa hapa yatakuwa kama mhimili wa yale yatakayojadiliwa katika sura za tatu, nne na tano. Dhana za tashbiha, istiari na taashira zimepambanuliwa kwa uwazi na aina za tamathali hizi kubainishwa.

### 2.2 Dhana ya Tashbiha

Neno tashbiha limetokana na neno lingine la Kiswahili au kitenzi "shabihi' lenye maana ya kufanana au kuwa sawa. Hii ni mbinu ya lugha inayotumiwa kufananisha au kushabihisha kitu kimoja na kingine. Ufananisho huu unaweza kuwa katika utendaji au hali. Tashbiha hufanya kazi endapo tu pana vitu viwili vinavyolinganishwa, ambapo kimoja hutumiwa katika kukirejelea na kuelezea kingine na aghalabu kimoja kati ya vitu hivyo huwa kinaeleweka na hivyo hutumiwa ili kuangazia hicho kingine.

Msokile (1993) asema kuwa tashbiha ni tamathali ya usemi ambayo huhusisha vitu vitatu:

i. Kizungumziwa
ii. Kifananishi
iii. Kiungo

Kizungumziwa ni kitu halisi ambacho huzungumziwa na kitu kinachofananishwa kwa fumbo. Kifananishi kipo katika mawazo na huzingatia maana iliyo dhahania. Kiungo ni sifa zipatikanazo katika kitu kinachozungumzwa. Kazi kuu ya kiungo ni kuhusisha vitu vyote viwili katika kuunda maana.

Kwa mfano: Umati ulipasua kicheko kilichosikika kama radi.

Katika mfano huu, kizungumziwa ni kicheko; kifananishi ni radi; na kiungo ni kile kitendo cha kusikia.

Tashbiha zinapotumika huweza kutambuliwa kwa matumizi ya maneno kama: 'kama', 'mfano wa', 'mithili ya', 'ja', na 'sawa na'. Kuhusu dhana hii ya tashbiha, Wamitila (2004) asema kuwa tashbiha ni misemo ya kilinganishi ambayo hukieleza kitu au sifa zake kwa kukilinganisha na kingine ili kuikuza sifa yake. Aendelea kusema kuwa, tashbiha huweza kuangaliwa kitaalamu kwa njia mbili kuu: Kwanza, tashbiha huweza kuangaliwa kama usemi wa kilinganishi ambapo vitu viwili hulinganishwa. Pili, tashbiha inaweza kuangaliwa kama usemi wa kilinganishi ambao unafumbata maana fulani. Njia ya pili ndiyo msingi wa kueleza tashbiha kama mojawapo ya tamathali za usemi. Kwa hiyo, ni hii njia ya pili tutakayoirejelea hasa katika utafiti wetu.

Leech (1969) asema kuwa tashbiha huwa na maana ya juujuu ikilinganishwa na jazanda ambayo huwa na maana ya ndani. Hata hivyo, Leech asema kuwa, tashbiha inaweza kudondoshwa kutoka kwa jazanda. Licha ya kuwa tashbiha huweza kudondoshwa kutoka kwa jazanda, Leech asema kuwa tashbiha huwa wazi kuliko jazanda kwa kuwa ina umahususi katika kulinganisha kwake ilhali jazanda imejaa utata. Maelezo haya ya Leech yanadokeza ni kwa nini katika kutumia jazanda kama tamathali ya usemi hatulinganishi moja kwa moja kinyume na tashbiha.

## 2.2.0 Aina Za Tashbiha

Kuna aina tatu kuu za tashbiha. Nazo ni: tashbiha wazi, tashbiha fiche na tashbiha ya kiutendi. Ufuatao ni ufafanuzi wa kila mojawapo:

### 2.2.1 Tashbiha Wazi

Aina hii ya tashbiha huwa na maana inayoeleweka moja kwa moja. Tashbiha ya aina hii aghalabu huwa na matumizi ya kivumishi ambacho ndicho huweza kuweka wazi maana.

Kwa mfano; Bakari ni mlafi kama fisi.

Katika tashbiha hii, kivumishi 'mlafi' ambacho ndicho msingi wa ulinganishi katika tashbiha hii kimeweka wazi tabia ya fisi ambayo imehamishwa kwa Bakari.

### 2.2.2 Tashbiha Fiche

Tashbiha ya aina hii huwa na maana isiyoeleweka kwa njia ya moja kwa moja. Uelewa mpana wa kilinganishi unahitajika na hili litafaulu katika kurejelea muktadha wake wa matumizi. Hii ni kwa sababu, kilinganishi kinaweza kuwa na hulka zaidi ya moja na hivyo huleta utata katika ufasiri wa maana pasi na kukikita katika muktadha wa matumizi.

Kwa mfano; Asha ni kama kinyonga.

Tashbiha hii ina maana zaidi ya moja. Mathalan, kilinganishi, kinyonga, ana sifa za kuwa kigeugeu na vilevile kufanya mambo polepole. Kwa hivyo, muktadha wa matumizi ya tashbiha hii ndio utakaotuwezesha kufasiri maana.

### 2.2.3 Tashbiha ya Kiutendi

Hii ni aina ya tashbiha ambayo imetolewa maelezo mapana. Wamitila (2003) asema kuwa, hii ni tashbiha ambayo hukuzwa na kuendelezwa kwa mapana, huweza hata kufikia mistari ishirini. Wamitila aendelea kusema kuwa, tashbiha ya aina hii hupatikana sana katika ushairi wa kiutendi. Hata hivyo, inaweza kupatikana katika mashairi ya tutumbi. Ufafanuzi huu wa tashbiha huunda taswira inayohusiana na kilinganishi kilichotumiwa.

Kwa mfano:

> Uko chini ya wazee wako tu, kama mtoto anayenyonya. Wazee wako wakulishe wewe; wazee wako wanilishe mimi. Mangapi hayo? Mimi sioni raha kulishwa na mtu ajinabi, si baba yangu wala si mume wangu; kama ni baba, basi ni baba yako. Tangu nimekuja hapa sikukuona kufanya kazi yoyote. Umekaa hapo huna hila yoyote, ukitaka pesa mbili – pesa mbili tu 'nobe' zinakushinda kuzivumbua, mpaka upewe...

Katika dondoo hili, Aziza, mkewe msimulizi, anamsuta mumewe kwa kuwategemea wazazi wake katika kila jambo. Hafanyi bidii yoyote kujitafutia ila kungoja msaada wa wazazi wake wamtunze yeye pamoja na mkewe.

Kwa hivyo, mumewe Aziza anafananishwa na mtoto anayenyonya kwani anawategemea wazazi wake kwa kila hali kama mtoto amtegemeavyo mamaye kwa kila hali.

**2.3 Istiari**

Sitiari ni mbinu ya kulinganisha vitu viwili au watu wawili moja kwa moja kana kwamba vitu na watu hao ni sawa kabisa. Kuhenga (1977) asema kuwa neno sitiari lilizaliwa kutokana na neno sitiri lenye maana ya ficha au funika. Kwa hivyo, sitiari ina maana ya kitu chenye kuficha. Kwa mfano: "Meno yenye weupe wa maziwa". Kifungu hiki kinaleta mfanano uliopo kati ya rangi nyeupe na maziwa. Christine alitabasamu kwa Peter ili Peter aone meno yake yaliyokuwa meupe sana. Istiari hii inadhihirisha urembo aliokuwa nao Christine – hasa meno yake yaliyokuwa meupe sana.

Kineene wa Mutiso (2005) ambaye anaiita sitiari kama istiari, asema kuwa, istiari ni mbinu ya kulinganisha vitu kwa kuhusisha vitu viwili tofauti kimaumbile na kitabia. Mlinganisho huu hauhusishi maneno kama vile ja, mithili ya, kama na visawe vyake.

Kuhusu dhana hii ya sitiari, Msokile (1993) asema kuwa, istiari hutumika katika hadithi kwa jinsi ambavyo maana ya masimulizi hujitokeza katika masimulizi mengine. Kwa mfano katika hekaya na hurafa, masimulizi hutolewa kwa kutumia wanyama kama wahusika na kila mnyama huwakilisha binadamu. Aidha, matendo ya wanyama wahusika husimamia matendo ya binadamu.

Kwa kuzingatia fafanuzi hizi, sitiari ni mlinganisho wa moja kwa moja ambao hutokea kwa kuhamisha maana ya sifa, tabia, sura, muundo au umbo fulani kutoka kwa kitu kimoja kwenda kwa kitu kingine. Kwa mfano: Ouma alikuwa simba mchezoni. Katika mfano huu, hulka za simba za ushujaa zimehamishwa hadi kwa Ouma ambaye alidhihirisha ushujaa mchezoni. Istiari ni tamathali ya semi ambayo kwa kiwango kikubwa inafanana na tashbiha ila hulinganisha vitu ama watu lakini bila kutumia viunganishi linganishi vya mithili ya, sawa na, na kama. Vitu au watu hulinganishwa na vitu au watu wengine kana kwamba vitu au watu hao ni sawa kabisa.

Lengo kuu la kutumia istiari ni kuonyesha uhusiano au ulinganisho wa vitu na watu tofauti tofauti katika kujenga uzito wa maana. Istiari huundwa na sehemu tatu: kilinganishi, kilinganishwa na msingi wa ulinganishi. Mambo haya matatu yanapaswa kuhusiana ndiposa ujumbe uliokusudiwa uweze kufasiriwa vyema. Maana inayojitokeza kutokana na istiari hutegemea muktadha wa matumizi ya istiari hiyo.

## 2.3.0 AINA ZA ISTIARI

Kuna aina kadhaa za istiari. Katika utafiti wetu, tulitumia aina chache ambazo kwa kiwango kikubwa ziliafiki uchunguzi wetu. Aina za istiari zilizotumika ni kama zifuatazo:

### 2.3.1 Istiari chakavu

Hii ni aina ya istiari ambayo kutokana na kuzoeleka kwayo, taswira ya awali iliyoifanya kuwa istiari haipo kutokana na mpito wa wakati. Istiari chakavu ni istiari ambayo imetumiwa sana katika lugha hivi kwamba haichukuliwi kuwa tamathali ya usemi tena bali inaonekana kama lugha ya kawaida. Matumizi ya istiari ya aina hii haileti athari za kisanii kwa hadhira kwani inaonekana kama maneno ya kawaida yaliyoeleweka.

Kwa mfano: Alikuwa na macho ya vikombe.

Istiari 'macho ya vikombe' ni istiari chakavu kwani imetumiwa sana na hivyo inaonekana kama lugha ya kawaida. Kuhusu aina hii ya sitiari, Wamitila (2008) asema kuwa istiari chakavu pia huitwa sitiari fifi na kuieleza kuwa ni ile ambayo hutokea pale ambapo taswira ambayo zamani ilieleweka kama istiari haichukuliwi hivyo tena labda hutokana na mpito wa wakati. Hii ni kumaanisha kuwa, istiari ya aina hii huwa imepoteza mshitukizo ambao ni muhimu katika istiari.

### 2.3.2 Istiari Kuu

Istiari ya aina hii hutawala kazi ya kifasihi kutoka mwanzo hadi mwisho. Hii ndiyo istiari inayobeba wazo kuu na kuendeleza maudhui ya kazi nzima ya kifasihi. Katika diwani ya *'Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine'*, hadithi *'Kanda la Usufi'* ni mfano mzuri wa istiari kuu. Asili ya sitiari hii ni methali: 'Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi.' Hii ina maana kuwa, matatizo yanayomsibu mtu mwingine, mwenzake huyaona kana kwamba si matatizo – hayachukulii uzito wowote. Anayeathiriwa ndiye anayeelewa uzito au ugumu wa jukumu linalomwandama. Katika hadithi hii, Sela apatapo ujauzito, linakuwa ni jukumu lake kuubeba mzigo wa kufukuzwa shuleni, nyumbani na kubeba lawama chungu nzima ilhali mwenzake – Masazu hauhisi mzigo huo. Aidha, wazazi wa Sela wanapambana na mzigo wa mwana wao kumshughulikia katika ujauzito na hata baada ya kujifungua ilhali wanajamii wengine wametulia makwao.

### 2.3.3 Istiari ya Kikaida

Hii ni aina ya istiari ambayo hufungamana na utamaduni wa jamii ilikochipukia. Kila jamii ina nyenzo zake za kifasihi za kujieleza, kuiasa jamii, kuonya, kuelimisha na kuburudisha. Nyenzo hizi za kifasihi ni pamoja na methali, nahau, tashbiha na istiari. Matumizi ya lugha katika jamii huegemea pakubwa mila na itikadi za jamii husika. Kwa mfano: nyingi za Kibantu zina msemo; 'Mungu si Athumani.' Msemo huu unazua istiari ambayo kulingana na jamii inamotumiwa, ina maana kuwa Mungu ni mkuu zaidi asiyeweza kufananishwa na binadamu. Kwamba uwezo wake Mungu ni wa upeo wa juu ukilinganishwa na ule wa binadamu. Kwa hivyo, sitiari hii inawaasa wanajamii walio ndani ya utamaduni huu kwamba wawe na imani kwa Mungu na wala sio kwa binadamu.

### 2.3.4 Istiari Hisimseto

Istiari hisimseto huweza kuhamisha hisia za kitu kimoja hadi kitu kingine. Mathalani, katika '*Damu Nyeusi*; tunaarifiwa kuhusu dereva mweupe mwenye moyo mweusi. 'Moyo mweusi' ni istiari inayoonyesha jinsi dereva huyu alivyokosa utu kiasi cha kumpita Fikirini licha ya kusimamishwa naye.

### 2.3.5 Istiari Sahili

Istiari sahili ni ile iliyo rahisi kueleweka kwa hadhira kwani msingi wa kilinganishi na kilinganishwa ni wa moja kwa moja. Hulka za kirejelewa zinashabihiana moja kwa moja na kilinganishi. Kwa mfano: Ali ni Sungura. Sungura kwa kawaida ana sifa za ujanja . Kwa hivyo, Ali akisemekana kuwa ni sungura ina maana kuwa Ali ni mjanja na haaminiki katika mambo yake.

### 2.3.6 Istiari Radidifu

Katika aina hii ya istiari, msingi wa kilinganishi na kilinganishwa si wazi bali huandamana na maelezo yanayolinganisha hali mbili. Kwa mfano, katika *'Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*,' 'donda' linalozungumziwa katika hadithi '*Maskini Babu Yangu*!, linaleta dhana ya istiari radidifu kwani msimulizi analinganisha hali ya kutotaka kukumbuka masaibu yaliyomsibu yeye na babu yake miaka mingi iliyopita kama donda. Asema:

> Sikutaka kutazama nyuma, kupiga darubini nyuma, kukumbuka nyuma, kujitonesha donda. Donda ndugu lililokataa kusikia dawa halina dawa mujarabu wala halikaribii kuwa na kovu. Donda tu, tena kubwa zaidi. Limejaa usaha na karaha na daima kunifanya kuhaha.

### 2.3.7 Istiari Mseto

Istiari ya aina hii huhusisha istiari kadhaa ambazo hutumiwa pamoja kurejelea hali moja. Katika aina hii ya sitiari, kilinganishwa kimoja hurejelewa kwa vilinganishi mbalimbali.

### 2.3.8 Istiari Changamano

Katika istiari changamano, huwepo istiari kadhaa ambapo istiari ya kimsingi huwa ni sahili na hutumika kama msingi wa istiari nyingine. Istiari ya aina hii ni changamano kwani inahusisha vilinganishi kadhaa au vilinganishwa kadhaa. Mfano: Mwanga huweza kuwa na maana ya ufahamu/uelewa.

### 2.3.9 Istiari ya Dhana

Wamitila (2008) asema kuwa, istiari ya aina hii hutokea pale ambapo kitu fulani kilicho katika mwanda maalum kinaeleweka katika muktadha au mwanda mwengine totauti. Yaani, ili kuwapo kwa aina hii ya sitiari kitu fulani kinaeleweka kwa misingi ya kitu kingine. Mfano: 'Wakati huruka' ni msemo ulio na maana ya mpito wa kasi sana wa wakati. Hapa, wakati ambayo ni dhana ya kidhanifu inapewa sifa ya kuruka kama ile ya ndege.

Pia, watu husema 'maisha ni safari' kwa maana kuwa kuna mengi ambayo mja huyapitia wakati anapoishi. Hali hii inalinganishwa moja kwa moja na hali ya kuwa safarini ambapo mengi hutokea tangu mwanzo wa safari hadi mwisho. Isitoshe, kuna sitiari isemayo 'wakati ni pesa'. Kikawaida pesa ni kitu cha thamani kwa binadamu. Kwa kusema wakati ni pesa kuna maana kuwa tutumie vyema muda tulio nao kwani tukiutumia visivyo huenda tukapata hasara.

## 2.4 Taashira

Taashira ni matumizi ya lugha ya ishara kuwakilisha ujumbe fulani ambapo jina au kitu fulani kinatumika kumaanisha kitu kingine chenye uhusiano na kile kilichotumiwa. Senkoro (1982) asema kuwa, taashira ni tamathali ya usemi ambapo jina la sehemu ya kitu kimoja au la kitu kidogo kinachohusiana na kingine kikubwa hutumiwa kuwakilisha kitu kamili. Kwa kutumia tamathali hii, msanii huunda maana mpya kabisa kwa mfano: Jembe huweza kutumika kuwakilisha mkulima, ikulu kuwakilisha raisi, kiti kuwakilisha kiongozi na pete kuwakilisha ndoa.

Akichangia maelezo ya dhana ya taashira hapo mwanzo, Leech (1969) asema kuwa , taashira ni ile maana ya kibunifu ambayo inahamishwa kwa kitu kutoka ile ya kawaida. Anaendelea kusema kuwa, baadhi ya taashira huwa ni jambo la kweli katika ukawaida wake. Kutokana na fafanuzi hizi kuhusu taashira, inabainika kuwa dhana hii humaanisha matumizi ya lugha ambapo maana ya kitu inayojulikana inahamishwa na kueleweka kivingine.

### 2.4.0 Aina za Taashira

### 2.4.1 Sinekidoki

Aina hii ya taashira hutumia sehemu ya kitu kusimamia kitu chenyewe. Mfano; Sikio la kufa halisikii dawa. Sikio hapa ni sehemu ya mwili ambayo imetumiwa kuwakilisha mwili mzima. Kwa hivyo, sikio ni sinekidoki inayosimamia mtu, kwa kuwa ni sehemu ya mwili mzima wa mtu.

Aidha, msemo 'kupata jiko' ulio na maana ya kuoa unazua taashira ya aina hii. Jiko ni kati ya vifaa vya jikoni vinavyotumiwa hasa na wanawake katika shughuli zao za upishi. Katika muktadha huu, jiko linaashiria baadhi ya majukumu ya mke kwenye nyumba- yaani upishi. Kwa hivyo, mtu kupata jiko ni taashira ya kuoa. Hali kadhalika, watu wasemapo kuhusu 'mkate wa kila siku' huwa na maana ya njia ya kujikimu. Mkate hapa ni sinekidoki inayosimamia chakula kwa ujumla wake au hali ya kujikimu kimaisha. Mkate, ambao ni sehemu tu ya vyakula vingi vilivyopo, unawakilisha dhana ya kijumla, chakula.

### 2.4.2 Taniaba

Katika taashira ya aina hii, mtu au kitu hurejelewa kwa kutaja tabia, sifa au hali ya mtu au kitu kingine. Sifa hizi na jina linalotumiwa lazima viwe vinajulikana na hadhira lengwa. Kwa mfano: Hitler na Iddi Amin ni viongozi waliojulikana kuwa na sifa za kidikteta katika uongozi wao. Kwa hivyo, mtu aitwapo kati ya majina haya, sifa zake zinabainika waziwazi. Aidha Samson ni jina la mtu katika Biblia aliyekuwa shujaa mkubwa. Mhusika katika kazi ya kifasihi apewapo jina kama hili ni ishara tosha ya nguvu na ushujaa.

Isitoshe, Firauni ni anwani ya wafalme wa zamani wa Misri waliokuwa katili sana. Kwa kurejelea jina hili, mhusika anayepewa jina la aina hii ana sifa za kutesa watu. Zaidi ya hayo, Musa ni nabii anayejulikana kuwakomboa Waisraeli kutoka utumwani Misri. Taashira ya aina hii inapotumika inabainisha wazi hulka za anayerejelewa kuwa na sifa za ukombozi kama vile nabii Musa.

### 2.4.3. Lakabu

Hii ni hali ya mtu au kitu kupewa jina lingine totauti na jina halisi. Majina haya aghalabu husheheni sifa za kirejelewa. Jina hili hupewa mtu kwa kurejelea sifa maalum. Wahusika mara nyingi huumbwa na msanii kwa kurejelea sifa hii ambayo huweza kuitwa mbinu ya majazi. Katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, hadithi *Mizizi na Matawi* imesheheni mbinu hii ya lugha. Mathalan, majina kama; Bi. Kudura na Sudi yamezingatia sifa hii. Pia, Duni, katika hadithi ya *Maeko* ni mfano mzuri wa lakabu kwani mwandishi anadhihirisha hili kupitia sifa za mhusika huyu ambaye ana sifa za mtu duni- asiye na thamani kwa sababu ya tabia yake mbaya.

## 2.5 Hitimisho

Katika sura hii, tumeangazia msingi wa kinadharia wa tamathali za usemi: tashbiha, sitiari na taashira. Tumechanganua mbinu ya tashbiha na aina zake. Vilevile, tumeangazia mbinu ya sitiari na kupambanua aina zake. Hatimaye, tumeshughulikia aina mbalimbali za taashira. Katika sura itakayofuata, tutashughulikia jinsi tamathali hizi za usemi zilivyotumika katika baadhi ya hadithi katika diwani ya '*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*'.

SURA YA TATU

# 3.0 MATUMIZI YA ISTIARI KATIKA DIWANI YA *DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE*

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, tutaangazia matumizi ya istiari katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Mbinu hii imetumika pakubwa kuelezea dhana mbalimbali kwa njia ya mnato wa kipekee. Hata hivyo, hadithi mbalimbali zimetumia mbinu hii kwa viwango mbalimbali. Baadhi ya hadithi zilizotumia mbinu ya istiari ni kama zifuatazo:

## 3.2 Samaki wa Nchi za Joto

Hadithi hii ni mojawapo ya hadithi za *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* ambayo imesheheni tamathali za usemi hususan sitiari. Katika ukurasa wa 14, mwandishi wa hadithi hii anaposifia urembo wa Christine, mhusika huyu (Christine) anasemekana kuwa na meno yenye weupe wa maziwa. Hili ndilo linalomfanya Christine atabasamu akitaka Peter ayaone menoye yaliyouzidisha urembo wake kwani weupe wa meno hayo unashabihishwa na ule wa maziwa. Aghalabu, weupe huu wa meno ya Christine ndio unaopelekea Peter kumpenda Christine.

Aidha, katika ukurasa huu huu (14), sifa za Miriam ambaye ni rafiki wa Christine zinapambanuliwa na Christine kama ifuatavyo ;

> Miriam alikuwa rafiki yangu Mtutsi ambaye labda Peter angempendelea zaidi. Nilijiambia. Alikuwa na wembamba na urefu waliopendelea Wazungu. Alikuwa pia na macho ya vikombe. Miriam hakuwa mwoga kama mimi. Hata alivuta sigara kadamnasi (uk.14).

Katika nukuu hii, ni bayana kwamba Miriam alikuwa mrembo kiasi cha kumpa Christine wasiwasi kuwa angeweza kumteka Mzungu makini akamuacha yeye Christine. Urembo wake, kati ya sifa nyingine, alikuwa na macho ya vikombe. Macho ya vikombe ni istiari inayodokeza uzuri wa umbo la mtu (msichana ) kupitia kiungo cha kuonea, macho. Ni dhahiri kwamba, uzuri wa macho yake uliuzidisha urembo wake.

Katika ukurasa wa 16, Christine anatupa taswira ya *'Sailing Club'*, mahali pa starehe ambapo aghalabu palijulikana kuwa pa Wazungu kwa sababu ya ada ya juu ya kiingilio iliyotozwa pale ambayo iliwafanya watu weusi washindwe kupamudu. Christine anasema;

> Kuwepo hapo kungenifanya niwe mweusi zaidi (uk.16).

Istiari hii ina maana kwamba, *Sailing club* ni mahali pa Wazungu (watu wanaojimudu) kwa hivyo Christine ambaye ni Mwafrika (watu wasiojimudu) hakutaka kupatikana pale kwani alikubali kuwa pale palikuwa mahali pa wenye vyao kama vile kina Peter.

Vilevile, sitiari imetumika katika ukurasa wa 17, ambapo Christine anapokuwa likizoni, yeye hajishughulishi kutafuta vibarua kama wanafunzi wenzake bali anajistarehesha tu bila kujali. Christine asema;

> Nilikuwa na miaka miwili ya kucheza michezo yangu; kujidanganya kuwa mtu mwingine au kuwa dubwasha tu (uk.17).

Hapa Christine anajilinganisha moja kwa moja na dubwasha au kitu kisicho na thamani. Thamani ya Christine imeshushwa na Peter (mpenziwe) ambaye, kinyume na matarajio, anaenda likizo Krismasi Nairobi peke yake. Kama Christine angekuwa na thamani yoyote kwa Peter basi wangeandamana kujivinjari pamoja kwani ni wapenzi. Jambo hili linamfanya Christine ajione duni hadi kufikia hadhi ya kujilinganisha na dubwasha.

Aidha, ukurasa huu huu (17) unadhihirisha matumizi ya sitiari pale ambapo Christine anajilaumu kwa masaibu yanayomwandama. Baada ya miezi kadhaa ya mahusiano ya kimapenzi na Peter, Christine anagundua kuwa amepata ujauzito. Hata hivyo, hathubutu kumwambia Peter kuhusu hali yake kwani jambo hili halikuwa katika mkataba wao wa siri. Kwa hivyo, Christine anajitwika jukumu la kushughulikia *"tatizo"* lake na ndipo anapomhusisha Margaret, dadake Miriam ambaye alikuwa mwuguzi kumsaidia kuavya ile mimba yake.

> Baada ya miezi kadhaa, niligundua nilikuwa mjamzito. Nilimwambia Miriam. Sikuthubutu kumwambia Peter. Sikudhani hilo lilikuwa lolote kwake. Halikuwa katika mkataba wetu wa siri. Huu ulikuwa msalaba wangu (uk.17).

Matatizo yanayomsibu Christine ya ujauzito na changamoto zake anayalinganisha na msalaba. Msalaba ni ishara ya mateso hasa kwa Wakristu. Imani ya Wakristu ni kuwa Yesu aliteseka kwa kuubeba msalaba kwa niaba yao. Katika muktadha huu, Christine yu radhi kuyavumilia mateso (msalaba) ili kuuhifadhi uhusiano wake na Peter. Alihisi kwamba kumwambia Peter kuhusu hali yake ya ujauzito kungeweza kukitia kitumbua cha uhusiano wake na Peter mchanga ndiposa akajitwika msalaba wake.

Isitoshe, matumizi ya istiari yanadhihirika katika ukurasa wa 19, ambapo tabia za Peter anapokuwa kazini zinashabihishwa na zile za mnyapara.

> Siku hiyo nilipompitia Peter ofisini, nilimkuta akiwasimamia wafanyikazi wake wakipakia mizigo katika lori, nje ya ofisi. Hapa alikuwa mnyapara hasa. Aliwatolea wafanyikazi wake amri kwa sauti ya juu (uk.19).

Mnyapara ni mtu anayewasimamia wengine kufanya kazi bila kujali maslahi ya wafanyikazi hao. Mara kwa mara, hutoa amri ambazo sharti zifuatwe kwa vyovyote vile. Christine anashtushwa na tabia hii ya unyapara ambapo hata yeye (Christine) hatambuliwi na mpenziwe. Ndiposa anasema, 'Hapa alikuwa mnyapara hasa'. Baada ya kuangalia jinsi istiari inavyojitokeza katika hadithi ya *Samaki wa Nchi za Joto*, hebu sasa tuyaangalie matumizi haya katika *Damu Nyeusi.*

### 3.3 Damu Nyeusi

Katika hadithi ya *Damu Nyeusi,* maudhui yaliyosheheni ni yale ya ubaguzi. Maudhui haya yameendelezwa pakubwa na lugha ya kitamathali iliyotumiwa. Istiari ni mojawapo ya tamathali za semi zilizotumiwa kwa ufanisi mkubwa katika hadithi hii. Hadithi inapoanza, mhusika mkuu, Fikirini yumo katika harakati za kungoja basi ili limpeleke chuoni alikokuwa akisomea shahada ya uzamifu katika somo la Kiingereza. Mara ya kwanza, Fikirini anajaribu kulisimamisha basi la abiria ambalo lilimwacha kwani dereva Mzungu alikaidi kulisimamisha. Hili ndilo linalomfanya Fikirini kuwa na hisia kuwa hata lingekuja basi lingine na liwe linaendeshwa na dereva Mzungu basi kama hapo mwanzoni, angeachwa.

> Chuoni si karibu lakini likija basi lingine na ambalo usukani wake umeshikwa na dereva mweupe mwenye moyo mweusi, yamkini mambo yatakuwa yale yale (uk.22).

Moyo mweusi wa dereva Mzungu ni istiari ambayo inaashiria moyo usio na uzuri. Inatarajiwa mtu mweupe kuwa na moyo mweupe ambao ni safi au wenye huruma. Hili ni kinyume na matarajio kwani dereva mweupe anatarajiwa kuwa mwenye moyo safi lakini mambo hapa ni kinyume.

Vile vile, katika ukurasa wa 23, Fikirini anapokuwa chuoni, kwa mara ya kwanza aligundua kuwa ni yeye peke yake aliyekuwa mtu mweusi katika darasa lao hivi kwamba mhadhiri Mzungu na wanafunzi wengine walishinda wakimsaili maswali ya kumdhalilisha na kumdunisha.

> Anakumbuka mara ya kwanza alipojikuta darasani yeye peke yake mweusi, kisiwa cheusi kwenye bahari ya weupe (uk. 23).

Katika nukuu hii, Fikrini anajilinganisha na kisiwa cheusi kwani ni yeye pekee Mwafrika aliyezungukwa na Wazungu (bahari ya weupe ). Hali hii inamfanya kudhahilishwa na kudunishwa kwani hana Mwafrika mwenzake wa kumtetea. Aidha, ukurasa wa 27, unadhihirisha matumizi ya istiari pale ambapo Fiona, yule dada aliyetaka kumpora Fikirini anapomuita Fikirini na Waafrika wengine kuwa tumbiri.

> Fala kabisa wewe, twawezaje sisi kuwa ndugu wa tumbiri kama nyie? Samahani (uk.27).

Hapa inadhihirika wazi jinsi ambavyo Wamarekani weusi wasivyotaka kujinasibisha na Waafrika. Licha ya asili yao ya Kiafrika, Wamarekani weusi huwadhalilisha weusi wenzao waishio Afrika. Isitoshe, katika ukurasa wa 29, Fiona anaposhindwa kufaulu kumpora alivyotaka anadai Fikirini akatwe "Mrija" kama adhabu ya kutishia kumbaka. Hapo awali Fiona alimtaka Bob amfyatulie risasi Fikirini lakini Bob akakataa.

> Hapana usimwache aende. Kama huwezi kufyatua risasi niachie mimi nimkate "mrija" (uk.29).

Mrija, kiuhalisia ni chombo chembamba chenye uwazi ndani. Katika muktadha huu, uume wa Fikirini umelinganishwa moja kwa moja na mrija pengine kwa sababu ya mfanano wao kiumbo.

### 3.4 Gilasi ya Mwisho Makaburini

Gilasi ya Mwisho Makaburini ni hadithi inayosimulia kuhusu vijana wanne; Msoi, Semkwa, Asha na Josephina ambao wana mazoea ya kwenda kujistarehesha katika *Baa ya Makaburini* hasa mwisho wa juma. Wakati huu, kama kawaida yao, wanaenda kujiburudisha licha ya onyo kutoka kwa Msoi ambaye alihisi pana hatari pale. Hatimaye wanavamiwa na majambazi wanaojifanya vizuu na kuporwa.

Masimulizi mengi kuwahusu marafiki hawa pamoja na shughuli zao yamefanikishwa pakubwa na matumizi ya tamathali za usemi hasa istiari. Mathalan, katika ukurasa wa 34, mwandishi anaposimulia kuhusu kubadilika ghafla kwa hali ya anga, anatumia istiari pakubwa .

> Njiani, mbingu ghafla ilikasirika - ikafinga uso wake mweusi. Kisha ikapasua mkonyezo uliotoa ufa mwembamba wa moto mwekundu na fedha. Kisha ikafuatia sauti kali ya mkemeo. Mbingu ilifanya hivyo mara moja tu. Tena bila kutiririsha hata tone moja la chozi. (uk.34).

Katika nukuu hii, istiari kadhaa zimetumika, mathalan, uso mweusi ni istiari inayoashiria mawingu meusi yaletayo mvua. Pia, ufa mwembamba ni istiari inayoonyesha kupiga kwa radi ambayo pia ni dalili ya mvua kubwa. Vile vile, moto mwekundu na fedha ni istiari ambayo inaashiria radi ambayo ni kitangulizi cha mvua kubwa. Aidha, sauti ya mkemeo ni ile sauti nzito inayoambatana na radi. Ni mngurumo unaoambatana na radi kabla ya kunyesha mvua kubwa. Isitoshe, tone la chozi ni istiari inayoonyesha mvua. Hii ina maana kuwa licha ya ishara zote za mvua, hapakunyesha hata mvua kidogo. Istiari hizi zote zinafafanua dhana moja kuu – mvua. Kwa hivyo, aina hii ya istiari ni ile ya istiari mseto kwani imehusisha istiari kadhaa ambazo zinarejelea hali moja.

Katika ukurasa wa 35, taswira ya mambo yalivyokuwa katika *Baa ya Makaburini* inaendelezwa vyema kwa matumizi ya istiari .

> Mambo hapo *Baa ya Makaburini*, kama nilivyosema, yalikuwa yanaingia sura. Bendi hai ilikuwa bado hata haijagongagonga. Muziki laini ulikuwa ukitumbuiza chini kwa chini. Ungedhani ukitoka kule makaburini (uk.35).

Muziki unalinganishwa moja kwa moja na kitu laini kinachoweza kumwongoa mja. Kitu laini huleta utulivu wa namna yake kama vile muziki laini unavyoweza kumwongoa mtu. Pia, ukurasa wa 36 unaendelea kuonyesha taswira ya mambo yalivyokuwa katika *Baa ya Makaburini* ambapo istiari iliyotumika inafafanua zaidi hali ya starehe iliyokuwa inashuhudiwa mle. Mwandishi anaeleza;

> Sasa usiku ulikuwa umeshafika kileleni, au tuseme umepevuka. Watu wamekula wameshiba.Wamekunywa hawajatosheka, maana kinywaji ni petroli ya muziki (uk.36).

Hapa, kinywaji kinalinganishwa na petroli ya muziki. Petroli ni mafuta yanayotumika katika baadhi ya vyombo vinavyokwenda kwa nguvu za moto. Kazi ya petroli ni kuongeza nguvu au kufanya kitu kipate nguvu zaidi za kukipeleka. Katika muktadha huu, kinywaji kimepewa sifa za kuongeza utamu wa muziki, kwamba utamu wa muziki utadumu iwapo mcheza ngoma atapata kinywaji.

### 3.5 Kikaza

Hadithi ya *Kikaza* inahusu uongozi wa Bwana Mtajika ambaye ni kiongozi katika kijiji cha Tekede. Bwana huyu anaongoza visivyo kwa kukiuka kaida za uongozi bora kama vile kuwa na ubinafsi, tamaa, ubaguzi na usaliti wa raia anaowaongoza. Mwisho wa haya ni kuporomoka kwa uongozi huu na kung`olewa mamlakani kwa viongozi. Dhamira na maudhui ya hadithi hii yameendelezwa kwa ufanisi mkubwa kupitia tamathali za usemi hususan istiari.

Anwani ya hadithi, *'Kikaza'* ni istiari. Kwa kawaida, kikaza huwa ni suruali ya ndani ya aina ya kipekee, ambayo hushonewa kiongozi kwa ushirikiano wa umma. Kimsingi, kikaza huchukuliwa kama nguo yenye heshima zake. Katika hadithi hii, neno kikaza limetumiwa kumaanisha uongozi au mamlaka. Kikaza kuweza kuvaliwa na kiongozi kwa ushirikiano wa umma ina maana kuwa uongozi hutokana na uchaguzi unaofanywa na raia, kwa hivyo, kikaza kimesimama kama kibadala cha uongozi.

Vilevile, ushonaji kikaza ambao ulifanywa na Bi Cherehani na Bwana Pima wakiwashirikisha raia wote ni istiari inayomaanisha uteuzi wa viongozi ambao hujumuisha raia wote. Iwapo patatokea shida katika uongozi, basi raia wote wanapaswa kujilaumu.

Isitoshe, katika hadithi hii, kuna hali inayodokeza hali ya kushindwa kulinda kikaza. Kushindwa kulinda kikaza ni istiari inayodhihirisha hali ya kushindwa kuhifadhi uongozi. Mwishoni mwa hadithi, hali hii inajidhihirisha kwa ambavyo Bwana Pima na Bi. Cherehani walivyochangia katika ushonaji wa kikaza naye Mtajika akajizuia kusema kasoro iliyokuwepo kwenye kikaza hicho. Hali hii inapelekea kupasuka kwa kikaza.

> Aliposhona (Bi.Cherehani) alifanya makusudi kupunguza kiwango alichopewa. Kikaza kikawa kinashika bila kusaza nafasi yoyote. Naye Mtajika kama alivyozoea kuota hakusema mpaka (kikaza) kilipokuwa kimepasuka (uk.48).

Kikaza kinapompasukia Bwana Mtajika ni istiari ya kushindwa kuhifadhi uongozi. Pia, katika ukurasa wa 45 wanakijiji wa Tekede, wanapojaribu kujitetea kwa wanavijiji jirani dhidi ya kuongozwa visivyo, wanasemekana kujitahidi kuuficha utupu wao wasichekwe na wanavijiji jirani. Utupu hapa ni kisawe cha uchi. Neno hili limetumika kistiari kwa maana ya aibu. Hapa, wanakijiji wa Tekede walijaribu kuificha aibu waliyokuwa nayo iliyoletwa na kiongozi wao. Waliuficha `utupu` huu kwa kufanyia mzaha fununu za uongozi mbaya zilipokuwa zikienea. Wangeeleza;

> Ni mapenzi tu, jambo ambalo mara nyingi wao husahau wakalieneza na kilionyesha ulimwengu. Mapenzi kikohozi yanapozidi, huja kama nguvu za sunami (uk.45).

Katika nukuu hii, wanakijiji wa Tekede wanapofanya mzaha kwa wenzao wanatumia istiari nyingine kwamba mapenzi ni kama kikohozi. Hii ni methali inayomaanisha kuwa uwapo ndani ya mapenzi ni vigumu kuificha hali hiyo kama ambavyo kikohozi kinapokuja hakifichiki. Wanadhihirisha kuwa mapenzi waliyo nayo kwa kiongozi wao ni makuu hivi kwamba ni muhali kuyaficha.

### 3.6 Maeko

Maeko ni hadithi inayosimulia maisha ya ndoa kati ya Duni na mkewe, Jamila. Jina halisi la Duni ni Hamduni lakini tangu utotoni mwake, watu walipendelea kumwita kwa ufupisho huu (Duni). Ndoa ya wawili hawa imekumbwa na masaibu si haba kwani Duni ni mlevi kupindukia na awapo mlevi humsononesha sana mkewe kwa kumtusi na kumpiga. Kwa sababu hii, watu mbalimbali wanamshauri Jamila kumwacha mumewe lakini Jamila anakaidi ushauri huu kwani licha ya mateso kutoka kwa Duni, kunayo mambo mazuri afanyiwayo na mumewe ambayo wanawake wengine hawafanyiwi na waume zao. Anakiri kuwa 'maeko' aliyomweka mumewe ndiyo yamfanyayo asimwache. Mwandishi asema:

> Basi baada ya yote haya, Jamila alijikuta kila siku akiyastahabu maisha ya ndoa yake na Duni na akichelea kuyakosa. Si kwamba hakusimanzika kwa shida azipatazo ndani ya ndoa hii lakini alikuwa akijipa moyo kwamba ni wanawake wangapi wa aina yake ambao wanafanyiwa anayofanyiwa na mume wake? Hakuwa na hakika ikiwa wanawake wenzake walioolewa walikuwa na shida kama zake lakini alijua kwamba wengi wao hawazipati starehe azipatazo (uk 56).

Dhamira na maudhui katika hadithi hii yamefanikishwa kupitia kwa tamathali za usemi zilizotumika. Miongoni mwa tamathali hizo ni istiari. Mwanzoni mwa hadithi, mwandishi anatupa taswira ya jinsi hali ilivyokuwa katika mtaa wa Sebleni alikoishi Hamduni na mkewe, Jamila. Wakazi wengi wa mtaa huu ni wafanyakazi wa ofisini ambao hutarajia utulivu wanapotoka kazini. Kinyume na hayo, wao hushuhudia zogo linaloletwa na Hamduni anapolewa. Mara kwa mara, huwabidi wakazi hawa kumwita Hamduni na kumwonya dhidi ya kuwasumbua awapo mlevi. Kumwonya kunaposhindikana, wao humtishia kipigo na kumshtaki. Hali hii inapambanuliwa zaidi kwa istiari katika usemi huu;

> Waliposhindwa kuyastahimili, walimwita mtiribu wao na kumweleza. Hili liliposhindwa kuwa dawa, walimtishia kipigo na kumshtaki (uk.50).

Dawa hapa, ni istiari inayorejelea suluhisho ambapo inasemekana kwamba Wanasebleni waliposhindwa kuibadili tabia ya Duni kwa kumwonya iliwabidi wamtishie kipigo na kumshtaki.

Aidha, jina Duni ni la kiistiari. Jina hasa la Duni ni Hamduni lakini tangu utotoni mwake, watu walipendelea kulifupisha. Alipokua na kuwa mtu mzima, tabia zake za ulevi na kuwasumbua wenzake zinamfanya aitwe Duni kwa jina na tabia.

> Naam, hivi ndivyo ambavyo Duni alikuwa akiisanifu Sebleni yake. Jina hasa la Duni lilikuwa ni Hamduni lakini tangu utotoni mwake, watu walipendelea kumwita kwa ufupisho huu. Sasa katika ukubwa wake, tabia zake za ulevi wa kupinduka zikamhalalishia kabisa kuwa Duni – kwa jina na maana (uk.51).

Katika ukurasa wa 51, watu mbalimbali wanapojaribu kumshawishi Jamila amuache mumewe, wanatumia istiari kujieleza. Mathalan, Jamila anamithilishwa na kinda. Kwa kawaida, kinda ni mtoto mchanga wa ndege. Kinda, kwa sababu ya thamani yake licha ya uchanga wake, hulindwa kwa hadhari mno ili asifikwe na hatari. Jamila anafananishwa na kinda kwa thamani aliyo nayo na kwamba anastahili kupewa ulinzi na malezi bora.

> Waliona kwamba Jamila hakuwa kamwe mwanamke aliyestahili kupatwa na yale iweje hasa, kinda kama Jamila apasaye kuita akaitikwa akatuma akatumikiwa, akubali kuendelea kusinginwa ndani na dume duni kama hili? (uk.51).

Vilevile, mume wa Jamila (Duni) anashabihishwa moja kwa moja na viumbe hasi kwa sababu ya tabia yake mbaya.

> Ndio maana mara kadhaa wamekuwa wakimwandama Jamila eti wanamhurumia, kwa kuendelea kudhikishwa na kuteswa na mume huyu mlevi, mbwa, kafiri, Firauni kwa miaka yote hii (uk.51).

Katika nukuu hii kwanza, Hamduni analinganishwa na mbwa. Katika jamii ya Waislamu mbwa ni mnyama najisi asiyethaminiwa hata kidogo. Kumfananisha Duni na mbwa ni sawa na kuonyesha jinsi ambavyo tabia za Duni zinavyomfanya asithaminiwe na watu.

Kafiri ni mtu anayekwenda kinyume na mafundisho na maadili ya Mwenyezi Mungu. Duni amelinganishwa na Firauni. Kimsingi, Firauni ni jina la cheo cha wafalme wa zamani wa Misri. Hata hivyo, jina hili hunasibishwa na mtu yeyote mwenye vitendo viovu. Duni anapoitwa Firauni, inaashiria utovu wake wa maadili ambapo huwaudhi watu wa Sebleni pamoja na kumuumiza mkewe kwa matusi na magumi.

Katika ukurasa wa 53, shoga ya Jamila, Ramla, anamuasa Jamila kulipiza kichapo cha mume wake kwa kumpiga pia. Katika hali hii, Ramla anatumia istiari kuliwasilisha wazo lake.

> "Enhe !"Shoga yake Ramla, alimshauri kwa balagha "wee hu kiwete, babu ee! Neno kwa neno, ngumi kwa ngumi. Kwa nini akukongeshe mtoto ungali mbichi hapo ulipo? Kwani kakununua?" (uk.53).

Katika nukuu hii, pametumika istiari – mbichi. Istiari hii ina maana ya kutoiva (kutokomaa). Hapa mwandishi wa hadithi hii ana maana kuwa Jamila ni mdogo kiumri na kwa hivyo hakupaswa kupitishwa matesoni kama alivyofanywa na mumewe, Duni.

Aidha, istiari nyingine imetumiwa kwenye ukurasa wa 54, ambapo Salim, rafikiye Duni, anajaribu kumshawishi Jamila amuache mumewe ili amuoe yeye. Salim anamdokezea Jamila kuwa amejaribu kumkanya mara nyingi dhidi ya tabia hii ya ulevi lakini katu Duni hakusikia maana mlevi si mtu.

> Nishamwambia Duni mara nyingi kwamba anavyofanya sivyo, lakini mlevi si mtu, shemeji (uk.54).

Hapa Duni kwa sababu ya ulevi wake, anachukuliwa kama mtu asiye na hulka za kiutu. Mtu aliye na utu hutarajiwa ajirudi anaporekebishwa lakini Duni, kwa sababu ya ulevi wake, anapoteza sifa hii kuu ya utu na ndiposa Salim asema, "Mlevi si mtu…"

Vilevile, Salim anapoendelea kumshawishi Jamila amuache Duni anatumia neno kama 'shetani' kumlinganisha Duni.

> Tafadhali niamini shemeji, kwamba kama utaweza kumkimbia shetani huyu basi mimi niko tayari kuenda na wewe popote (uk.54).

Hapa, Duni anamithilishwa na shetani kutokana na vitendo viovu amfanyiavyo mkewe, Jamila. Kwa kawaida, shetani ni kiumbe anayeaminika kuendeleza vitendo viovu. Kwa kumlinganisha Duni na shetani, Salim anaamini kuwa Jamila atatishika na kushawishika kumuacha mumewe.

Isitoshe, nyumbani kwa Jamila na Duni kunamithilishwa na jahanamu. Kimsingi, jahanamu ni mahali maalum ambapo inaaminika kuwa watu wasiotii maagizo ya Mungu huenda baada ya kufa. Taswira ya jahanamu si nzuri na mahali panapoaminika kuwa na aina ya shida kama adhabu kwa waliomwasi Mungu walipokuwa wakiishi duniani. Katika hadithi hii, Salim anapaita nyumbani pa Duni na Jamila kuwa ni jahanamu kwa kurejelea mateso anayoyapitia Jamila akiwa pale. Salim anamtaka Jamila apaambae mahali pale ili amuoe.

> Nakuhurumia na nakupenda shemeji. Kwa nini huikimbii jahanamu hii? (uk.54).

Kwa upande wake, Jamila anayapinga matakwa ya Salim ya kumuacha mumewe kwa kutumia istiari zifuatazo: Kwanza, Jamila anamhakikishia Salim kwamba asije akadhani amekosa mapenzi ya mume wake. Anaendelea kujisemesha kwa kutumia methali ya kistiari kwamba usilolijua ni usiku wa kiza. Methali hii ina maana kwamba, jambo ambalo hulijui huwezi kulielewa vyema. Katika muktadha huu, Salim hajui mapenzi anayoyapata Jamila kutoka kwa Duni na kwa hivyo hakupaswa kwa vyovyote kuhukumu mapenzi hayo ili kujinufaisha yeye. Isitari hapa ni usilolijua ni usiku wa kiza. Jambo usilolijua limemithilishwa moja kwa moja na usiku wa kiza. Katika usiku wa kiza, ni vigumu mtu kuona na kwa hivyo, ni vigumu kwa Salim kuona kuwa ndoa kati ya Jamila na Duni ilikuwa na mapenzi tele .

Isitoshe, Jamila aambiwapo na Salim aitoroke jehanamu ile, anauliza swali la balagha kuwa iwapo pana uwezekano wa kupapata mahali palipo na starehe wakati wote kama vile peponi.

> Ni kweli kwamba usilolijua ni usiku wa kiza, yaani kama hii ni jahanamu, iwapi hiyo pepo nyingine katika hii dunia? (uk.54).

Mwandishi pia ametumia istiari katika ukurasa wa 50 asemapo;

> Basi kutokea hapo, ikawa hakuna aliyemshughulikia tena zaidi kawaida tu ya kumlaani na kumwapiza : Mja wa laana, mlevi, mbwa na mengine kadha wa kadha ambayo yote, hapana shaka yalikuwa ni dua ya kuku, haimpati mwewe (uk.50).

'Dua ya kuku haimpati mwewe' ni methali iliyo na maana kwamba kero la mnyonge halimwathiri mwenye nguvu. Katika muktadha huu, kero za Wanasebleni zinafananishwa na dua la kuku ilhali mwewe ni Duni ambaye haathiriwi na kero hizo. Licha ya lawama na matusi kutoka kwa Wanasebleni, Duni hakurekebisha tabia yake bali alizidi kuwaudhi wenzake.

### 3.7 Kanda la Usufi

Hadithi hii inahusu maisha ya vijana wawili: Sela na Masazu ambao wanajiingiza kwenye mapenzi wangali shule ya upili. Hali hii inampelekea Sela kupata ujauzito na kulazimika kuacha shule kwa muda ili kumtunza mwanawe. Baada ya kumaliza masomo yao ya shule ya sekondari, wawili hawa wanaamua kuishi pamoja kama mume na mke. Hata hivyo, kwa sababu ya uchochole wao, wanashindwa kuimudu gharama ya kumchukua mtoto kwa kufuata taratibu zilizowekwa na hivyo, inawabidi wapange njama ya kumwiba mtoto usiku, jambo linalopelekea kutokea mauti yao kupitia kusombwa na mafuriko.

Mwandishi amefaulu pakubwa kujieleza kupitia matumizi ya istiari miongoni mwa tamathali nyingine. Kwanza, mwanzoni mwa hadithi (uk60), Sela anasemekana kuwa na moyo mwepesi. Moyo mwepesi ni istiari inayomanisha hali ya kuwa na huruma. Sela anamhurumia Masazu anapojifanya kuwa mgonjwa. Mwandishi anasema yafuatayo kumhusu Sela.

> Sela aliingia katika mtego. Moyo wake mwepesi ulimsaliti. Moyo wake daima uliyeyushwa na huruma alipomuona mja akiteseka. Alibaini alikuwa na wajibu wa kiutu (uk.60).

Pia, anwani 'Kanda la usufi' ni ya kiistiari. Anwani hii inatokana na methali 'Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi'. Hii ina maana kuwa, matatizo yanayomkumba mwenzio huonekana kama jambo rahisi kwako na kwa wengine. Yule anayeyapitia matatizo hayo ndiye anayehisi uzito wayo. Hapa Sela na familia yake ndio wanaohisi uzito wa masaibu yanayowakumba. Mathalani, Sela anapopata ujauzito, ndiye anayeathirika zaidi kwa kufukuzwa shuleni, kufukuzwa nyumbani na kusitisha masomo yake. Masaibu ya Sela yanalinganishwa moja kwa moja na kanda la usufi. Kulingana na watu wengine, matatizo ya Sela ni mambo rahisi na ya kawaida. Lakini Sela mwenyewe ndiye anayefahamu uzito wa masaibu yanayomwandama.

Aidha, katika ukurasa wa 62, Sela na wenzake wawili wanapoitwa ofisini mwa mwalimu mkuu baada ya kugunduliwa kuwa wajawazito, wanalemewa na mawazo kwani hawakujua ambalo lingefuata baada ya mkutano wao na Mwalimu mkuu. Mwandishi asema:

> Ingawa walifahamu sababu ya kuitwa pale, mpango uliokuwepo ulikuwa usiku wa giza (uk.62).

Hapa, mpango unalinganishwa moja kwa moja na usiku wa giza. Kwenye usiku wa giza, mtu hawezi kuona kilicho mbele yake. Katika muktadha huu, mambo waliyopangiwa na mwalimu mkuu hawakuyafahamu katu kama vile ambavyo mtu hawezi kuona kwenye giza.

Isitoshe, katika ukurasa wa 63, mwandishi anaonyesha hali ilivyokuwa kwa Mzee Butali baada ya kupokea habari ya ujauzito wa Sela. Asema; 'Boma la mzee Butali liligeuka jahanamu baada ya kutoka shuleni'.

Hapa, boma la mzee Butali linalinganishwa moja kwa moja na jahanamu –mahali panapokisiwa kuwa pabaya na palipojaa mateso. Jahanamu ni mahali ambapo kiuhalisia, hapakaliki! Hapa palikuwa jahanamu hasa kwa Sela na mamake ambao walifurushwa kwa kuamriwa na Mzee Butali kuondoka .

Isitoshe, Mzee Butali anapogombana na mkewe kuhusu Sela kupata mimba, mamake Sela anamuasa mumewe kuwa wasilaumiane kwani janga hili ni lao wawili kwani ndio wazazi wa Sela. Sela analinganishwa na maradhi. Maradhi ni istiari inayotokana na msemo unaotumiwa kulalamikia tabia mbaya za mtoto ambapo mzazi hushangaa iwapo alizaa au alitoa maradhi tumboni. Mama Sela asema:

> Baba Sela, nani kasema huu ni msiba wangu? Tutautwaa pamoja. Huyu ni mtoto wetu, sio maradhi (uk.63).

Pia, neno 'msiba' limetumika kiistiari. Istiari hii inatumiwa na mamake Sela anapomsuta mumewe dhidi ya kumbagua mwana wao kwa sababu ya kupata ujauzito akiwa angali shuleni. Msiba kwa kawaida ni jambo liletalo dhiki hasa kutokana na kufiwa. Katika muktadha huu, msiba inaashiria janga alilolileta Sela katika familia yao hasa kwa wazazi wake.

### 3.8 Tazamana na Mauti

Hii ni hadithi inayosimulia jinsi msichana, Lucy anavyotamani maisha ya Uingereza. Anawazia njia mbalimbali za kumfikisha huko na hatimaye anapata bahati ya kuolewa na Mzungu, Mr. Crusoe ambaye anaitimiza ndoto ya Lucy ya kuishi Uingereza. Tamaa ya Lucy ya maisha mazuri huko Uingereza haidumu kwa muda mrefu kwani anapata ajali na kufariki dunia pindi tu anapoahidiwa urithi na Mr.Crusoe.

Tamathali za usemi zilizojumuishwa na mwandishi wa hadithi hii ili kuifanikisha kazi yake ni pamoja na istiari miongoni mwa tamathali nyingine. Mathalan, mwanzoni mwa hadithi (uk 91), Lucy anaposifia Uingereza, hataki yeyote kukosoa sifa za Uingereza na iwapo yeyote angethubutu kufanya hivyo, Lucy angemfananisha na kisa cha sungura na zabibu :

> Mambo si hayo! Usije kabisa ukamwambia Lucy kuwa hiyo yake ni ndoto tu. Atagombana na wewe na kukwambia wazi kwamba wewe umegeuka sungura aliyezikosa zabibu (uk.91).

Hapa, sungura mwanzoni alitamani sana zabibu lakini alipozikosa, alijidai kuwa hakuzitaka kwani si tamu! Katika muktadha huu, Lucy anawalinganisha wale wanaoidharau Uingereza kuwa ni sungura (wanatamani kufika huko lakini wamekosa fursa). Zabibu zinalinganishwa moja kwa moja na maisha matamu ya Uingereza.

Aidha, istiari nyingine inajitokeza pale ambapo Lucy anazidi kujipa moyo kuwa siku moja itafika ambapo ataishi Uingereza. Hakatishwi tamaa na jinsi siku zinavyojikokota. Kwake yeye liwe liwalo, Uingereza ataifika siku moja

> Yeye anaamini siku moja itakuwa siku, maana hizi zote ni mafigu tu, hazishi kuporomoka! (uk.91).

Lucy analinganisha siku na mafigu. Hii ina maana kuwa, siku huweza kuyoyoma kwa kasi kama vile mafigu. Anajipa moyo kuwa hata siku zikijikokota zitapita hatimaye na ndoto yake ya kwenda Uingereza itatimia.

Vile vile, sababu zinazompelekea Lucy kuipenda na kuienzi Uingereza ni pale anapolinganisha Uingereza na nchi yao, anahisi kuwa Uingereza kuna maisha mazuri ikilinganishwa na kwao. Anailinganisha nchi yake na nchi ya Firauni. Kulingana naye, nchi ya Firauni ni nchi ya mateso na isiyo na uzuri wowote. Firauni ni anwani ya wafalme wa zamani wa Misri ambao walitajika kwa kuwatesa raia wao. Isistoshe, katika nchi ya Firauni hakuna ajira hata ya mshahara mdogo. Ndiposa Lucy analinganisha ajira ya malipo duni na kazi ya tonge la ugali. Msemo huu, tonge la ugali umetumika kiistiari kumaanisha kazi yenye mshahara duni ambayo hata haipatikani katika nchi ya kina Lucy:

> Anajua kwamba hapa pao nchi ya Firauni, siku hizi hangepata hata hiyo kazi ya tonge la ugali, sikwambii muluki (uk.91).

Jambo hili (ajira) ndilo linalomchochea Lucy kuipendelea Uingereza, kwani kinyume na kwao, Uingereza ni nchi inayojali maslahi ya raia wake hususan kuwapa ajira yenye mishahara mizuri ya kuwawezesha kuyamudu vyema maisha.

Katika ukurasa huu huu wa 91, Lucy anaposifia Uingereza na uzuri upatikanao kule, anapaita peponi. Peponi kwa kawaida ni mahali panapodhaniwa kuwa pa starehe na mazuri yote hupatikana huko. Lucy analinganisha Uingereza moja kwa moja na peponi ambapo anatafuta mbinu yoyote ile ili afanikiwe kupaishi. Anajisemea:

> Lini angepata nafasi ya kupenya kwenye chungio na kudondokea Uingereza? Aaa – ni peponi Uingereza (uk.91).

Isitoshe, Lucy anawasuta wale wanaoiharibia sifa Uingereza. Kulingana na yeye, Uingereza inastahili sifa zote nzuri kwani mambo yanayofanyiwa raia wake ni ya kuwaridhisha. Mathalan, kupewa nyumba na makazi, kupewa mshahara bila ya kufanya kazi, kupewa vifaa vya nyumbani : Televisheni, friji, jiko la umeme, mapazia, mazulia, nguo na mavazi. Lucy anasema;

> Watu wengine ni wachoyo tu, wale wanaojaribu kuipaka rangi mbaya Uingereza. Eti wanaiita jahanamu (uk.92).

Hapa, watu wanaoilinganisha Uingereza na jahanamu wana maoni kuwa Uingereza ni mahali pabaya. Jahanamu ni mahali panapoaminika kuwa watu ambao walikuwa watenda dhambi wakishafariki dunia huenda huko ili kuyafidia makosa yao kwa kupata mateso. Kinyume na hili, Lucy anaamini kuwa Uingereza ni peponi – mahali pazuri.

Zaidi ya hayo, katika ukurasa wa 95, Lucy ashaizoea Uingereza na maisha yake ya kifahari na anajiona kuwa ameshakuwa mtu mkubwa. Mtu mkubwa ina maana ya mtu mwenye nafasi katika jamii haswa katika masuala ya kiuchumi. Kwa sasa, Lucy ameingia tabaka lingine la watu wakubwa. Mwandishi asema;

> Baada ya kujifundisha kuendesha gari, humtembeza na kumpeleka popote wanapoamua wao wawili kwenda, mara nyingi, mwahala mwa mapumziko wanamokwenda watu wakubwa kama wao.Yeye sasa ameshakuwa mtu mkubwa. Ala! Kwa nini ajitupe? (uk.95).

Pia, mwishoni mwa hadithi, Lucy anapoahidiwa urithi na mzee Crusoe, anaingiwa na hamu kuuzunguka mji wa London ili kusherehekea utajiri wake akiwa angali mdogo kiumri.

> Alitembea jiji hilo kuliambia kwamba msichana mbichi na tajiri anakuja ili jiji lijitayarishe kumpokea hatimaye (uk.96).

Hapa, Lucy analinganishwa moja kwa moja na msichana mbichi. Kitu kibichi ni kile kisichokomaa au kuiva. Hapa, licha ya umri mdogo wa Lucy, amepata utajiri mkubwa ambao hautarajiwi kuwa na msichana wa umri wake. Lakini kwa bahati mbaya, Lucy anaishia kupata ajali na kufariki dunia pasi na kuifikia ndoto yake ya kuirithiwa mali ile.

### 3.9 Hitimisho

Katika sura hii, tumezipitia istiari mbalimbali kama zilivyotumika katika diwani ya damu nyeusi na hadithi nyingine. Tumegundua kwamba, zipo aina nne kuu za istiari zilizotumika kwa wingi katika diwani hii. Aina za istiari hizi ni kama zifuatazo: istiari chakavu, istiari kuu, istiari hisimseto na istiari mseto. Hata hivyo, kuna aina za istiari zilizotumika kwa uchache kama vile istiari changamano na istiari ya dhana.

## SURA YA NNE

## 4.0 MATUMIZI YA TASHIBIHA KATIKA DIWANI YA *DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE*

### 4.1 Utangulizi

Tashbiha, kama ilivyofafanuliwa katika sura ya pili, ni mojawapo ya tamathali za usemi zinazotumika kulinganishia vitu, hali au dhana mbalimbali. *Damu nyeusi na Hadithi Nyingine* ni mkusanyiko wa hadithi zilizosheheni pakubwa mbinu hii. Waandishi mbalimbali wa hadithi hizi wametumia tashbiha katika kuwasilisha kazi zao. Lengo la sura hii ni kudhihirisha matumizi ya tashbiha katika hadithi teule zipatikanazo katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* vifuatavyo:

### 4.2 Samaki wa Nchi za Joto

Mwanzoni mwa hadithi hii, Christine anapoelezea kuhusu uhusiano wake na Peter, anaulinganisha na uhusiano wa watoto wanaokwenda shule. Hapa, Christine anamaanisha kuwa, watoto waendapo shuleni huwa hawaendi kwa hiari yao bali huwabidi kufanya hivyo kwa sababu ya matarajio ya jamii. Kwa Christine, uhusiano wake na Peter ulikuwa wa hiari japo haoni sababu kuu ya uhusiano huo ambao haukuonekana kuelekea popote pazuri.

> Uhusiano wetu niliuona kama kitendo cha watoto kwenda shuleni, jambo walitendalo tu kwa sababu hawana budi (uk11).

Tashbiha inayojitokeza hapa ni uhusiano kati ya Christine na Peter ambao unalinganishwa na kitendo cha watoto kuenda shuleni, jambo ambalo huwabidi kulifanya. Pia, mwandishi anamtumia mhusika Christine kuelezea umbo la Peter anaposema:

> Peter alikuwa na umri wa miaka thelathini na mitano tu ambayo kwangu – kutokana na umri wangu wa miaka ishirini, nilimuona mkongwe sana. Hata hivyo, akiwa na bombo aliyoipenda sana, alionekana kama mvulana wa miaka kumi na minne. Alikuwa na maungo mviringo ya ujana, mwili laini kama wa mwanamke, na miguu iliyobonyea na iliyopuuka. Ulaini wa ngozi yake ulikuwa sawa na wangu (uk11).

Hapa, licha ya umri mkubwa wa Peter, analinganishwa na mvulana wa umri mdogo. Aidha, Peter anaonekana na maungo mviringo ya ujana japo yeye si kijana. Isitoshe, mwili wa Peter unalinganishwa na ule wa mwanamke kwa kuwa ni laini sana. Vilevile, ulaini wa ngozi ya Peter unamithilishwa na ulaini wa ngozi ya Christine. Hii ina maana kwamba, licha ya umri mkubwa wa Peter, yeye bado anaonekana mdogo kiumri pengine kutokana na malezi bora.

Aidha, Christine na Peter, walipokuwa chumbani mwa Zac, Peter anaonekana kuvutiwa na chumba hiki. Mwandishi anasema:

> Peter alionyesha kuvutiwa na chumba uchwara cha Zac. Alitazama kila kitu kwa makini kama wafanyavyo watalii (uk 11).

Katika dondoo hii, umakinifu wa Peter katika kukikagua chumba cha Zac unamithilishwa na jinsi watalii watazamavyo vitu kwa umakini.

Pia, katika hali ya kujuana pale kwa Zac, Peter anamuuliza Christine kuhusu kozi anayosomea kule chuoni. Anauliza Christine kama vile mjomba mkarimu awezavyo kumuuliza mpwa wake.

> Peter aliuliza kama mjomba mkarimu anavyomuuliza mpwa wake (uk13).

Peter analinganishwa na mjomba mkarimu. Mjomba kwa kawaida ni jamaa anayejali sana maslahi ya mpwa (mtoto wa dadake). Naye Christine analinganishwa na mpwa. Hulka kuu ya mpwa kwa mjombawe huwa ni utiifu. Kwa hivyo, Christine anapoulizwa kuhusu masomo yake na Peter anajibu kwa utiifu.

Aidha, tashbiha nyingine inajitokeza pale mtaa wa Tankhill ambapo Peter na mwenzake wa Kizungu walikuwa wakiburudika kwa nyama choma na mvinyo. Hawakuwa na wasiwasi wowote licha ya kuwa walikuwa wageni. Mwandishi asema:

> Hapo ungewaona wamekalia viti vya plastiki wakinywa bia na wengine wakitafuta makahaba. Hapa walijifanya kuishi kama wenyeji (uk.16).

Hapa, maisha ya Wazungu hawa yanalinganishwa moja kwa moja na ya wenyeji kwa kuzingatia mahali wanamofanyia starehe zao na hata wale makahaba wanaowatafuta. Starehe zenyewe na hata vyakula na vinywaji vilishabihiana na vile vya wenyeji.

Baada ya uhusiano wa muda wa kimapenzi kati ya Christine na Peter, Peter alianza kuonyesha kutomjali Christine na hili linamfanya Christine kujihisi kuwa hana thamani tena. Christine asema :

> Badala ya kujihisi salama, niliingiwa na wazo la kuwa kama debe tupu (uk.17).

Hapa Christine anajilinganisha na debe tupu - kitu kisichokuwa na thamani yoyote. Anajiona kukosa thamani hasa kutokana na kutokumjali kwa Peter. Aidha, Peter anapopanga kusafiri kuenda Nairobi Krismasi ya mwaka huo, anamuaga mpenziwe Christine kwa kumpiga busu shavuni kadamnasi ya watu. Umati unapoyaona haya, unaghadhabishwa na hali hii na kucheka kicheko cha dhihaka ili kumsuta Christine kwa kukosa maadili.

> Umati , ulipasua kicheko nilichokisikia kama radi (uk 17).

Kicheko hapa kinafananishwa na mpigo wa radi. Hii ni kuonyesha jinsi kilivyomshtua Christine na jinsi kilivyokuwa kikubwa na cha sauti ya juu. Isitoshe, Christine anapopanga kuolewa katika familia ya kitajiri, ana imani kuwa atafaulu kwani ana elimu ya kutosha ambayo itawavutia wanaume matajiri. Anasema ;

> Nikiwa na shahada ningekuwa kama ng`ombe wa Kizungu … Friesian au Jersey sio wale wa Ankole wenye pembe zilizojitea ovyo (uk.17).

Hapa Christine anajilinganisha na ng`ombe wa Kizungu (Friesian au Jersey ) ambao thamani yao huwa ya juu ikilinganishwa na ng`ombe wa kienyeji (Ankole). Peter alipokuwa akifanya biashara ya magendo na Jagjit, Peter alionekana akiikagua kwa uangalifu noti moja ya dola za Kimarekani iliyokuwa bandia.

> Aliiangalia kwa makini kama mwanasayansi aliyekuwa akifanya uchunguzi maabarani (uk.18).

Umakinifu wa Peter katika kuchunguza ile noti unalinganishwa na umakinifu wa mwanasayansi anapofanya uchunguzi katika maabara. Hii ina maana kuwa Peter alimakinika sana.

### 4.3 Damu Nyeusi

Hii ni hadithi iliyosheheni tamathali za usemi hususan tashibiha. Maswala yanayoangaziwa katika hadithi hii yanapewa uzito zaidi kupitia mbinu hii ya tashibiha. Mathalan, mwanzoni mwa hadithi, mwandishi anatoa usimulizi wa hali mbaya ya anga Marekani na mbinu za kukabiliana na hali hiyo. Inabidi mtu avae nguo nyingi na nzito na vivyo hivyo, viatu vizito ambavyo vinamithilishwa na vile vya wanajeshi ili asiweze kuathiriwa na baridi hiyo kali.

> Lo! Mtu sharti avae safu ya maguo na maguo na soksi nzito pamoja na viatu, viatu vizito kama vya wanajeshi wa nchi kavu (uk.22).

Viatu vya wanajeshi, kama yalivyo mavazi yao mengine kwa kawaida huwa vizito ili kuwakinga na hali ngumu wanazozipitia wakilinda nchi. Viatu hivyo vimemithilishwa na vile vivaliwavyo Marekani wakati wa msimu wa baridi ili kuonyesha athari ya hali hiyo mbaya ya anga.

Fikirini anapotembea kando ya barabara kwenye kijia cha wapita njia, mwandishi anaeleza jinsi alivyotembea kwa kupepesuka na hivyo mwendo wake kulinganishwa na wa mtu aliyelewa chakari. Asema;

> Alitembea kando ya barabara kwenye kijia cha wapita njia huku anyapianyapia nyapunyapu na kupepesuka pepesupepesu kama mlevi chakari (uk 22).

Mtu alewapo kupita kiasi hukosa udhabiti hasa anapotembea na kwa hivyo, Fikirini anapepesuka sio kwa sababu ya ulevi bali kwa kuhakikisha amepita kijia hicho kidogo cha wapita njia asije akapatikana na hatia nyingine ya kukanyaga pasipofaa.

Pia, mwandishi anatumia tashbiha pale anaposimulia kuhusu mazingira ya Marekani kwa wakati huo. Theluji inasemekana kufunika kila kitu kama blanketi la unga lililoufunika mji. Kwa kawaida, blanketi linajulikana kutumiwa kujifunika ili kujisetiri na baridi hasa wakati wa usiku. Hapa, theluji imepewa sifa za blanketi za kuweza kuufunika mji. Hii ina maana kuwa, theluji ilikuwa imetapakaa kote:

> Theluji ilikuwa imefunika kila ncha na kujenga mandhari nyeupe pepepe. Si madirisha, si milango, si paa, si kuta, si majani ya miti, si matawi na mashina, si kando na katikati ya barabara ya magari, si pembezoni na katikati ya vijia vya wapita njia na waendeshaji baiskeli – kote weupe wa theluji umehanikiza na kufunika kila kitu kama blanketi la unga lililoufunika mji (uk 22).

Vile vile, Fikirini anapokuwa chuoni, anapitia dhuluma si haba kutoka kwa wanafunzi wenzake na hata wahadhiri. Jambo hili limempa funzo kuwa hakuna mahali pazuri kama nyumbani hata pawe pangoni. Dhuluma na ubaguzi anaoupitia katika nchi ngeni hauwezi katu kulinganishwa na ukarimu na utu nchini kwao. Ndiposa mwandishi asema ;

> Tangu hapo ameendelea kuwa mwanafunzi mzuri wa chuo cha maisha ya Marekani. Amejifunza kuwa hakuna mahali kama nyumbani. "Nyumbani ni nyumbani ingawa pangoni" (uk.23).

Isitoshe, wanafunzi wenza na wahadhiri wa Fikirini walikuwa hawasiti kumsaili maswali kumdhalilisha na kumdunisha. Kati ya maswali ya kumdhalilisha aliyoulizwa ni;

> "Je mwaishi kwenye miti kama tumbiri?"(uk.23).

Kwa kawaida, tumbiri ni wanyama wanaojulikana kwa kuishi mitini. Kwa kumuuliza Fikirini iwapo wao wanaishi mitini kama tumbiri ni kuwadhalilisha Waafrika kuwa wao ni kama wanyama (tumbiri).

Isitoshe, mwandishi anatumia tashbiha kueleza jinsi Fikirini alivyoingiwa na uoga wakati alipokumbana na wale majambazi wawili – Fiona na Bob. Walipotaka kumpora, walimwamuru kuzivua nguo zote alizokuwa amevaa la sivyo wangemuua.

> Fikirini alizibwaga nguo moja baada ya nyingine huku akitetemeka kama majani ya mgomba kwenye dhoruba (uk 27).

Kutetemeka kwa Fikirini kunafananishwa na jinsi majani ya mgomba yafanyavyo hasa wakati wa upepo mkali. Hii inaashiria woga uliomgubika Fikirini. Zaidi ya hayo, Fikirini anapokumbana na majambazi hawa, Bob na Fiona, wanapogundua kuwa hakuwa na pesa za kumpora, Fiona anaamuru Bob amfyatulie risasi Fikirini na kumuua. Jambo hili linamshtusha sana Fikirini na analia sana. Mwandishi anatumia tashbiha kuieleza hali hii:

> "Please no! Don`t kill me brother," Fikirini alisihi huku akilia machozi kama kitoto kidogo (uk 29).

Kwa kawaida, ni nadra kwa mtu mzima kulia lakini hapa mambo yalikuwa yamemfika kooni Fikirini na ikambidi alie kama waliavyo watoto wachanga.

Isitoshe, Fikirini anapojaribu kujitetea kwa kina Fiona na Bob ili wamwonee imani kwa kuwa wao ni watu wamoja Waafrika, Fiona kwa mara nyingine anamkana na kumlinganisha na tumbiri. Kwa kumfananisha na tumbiri, Fiona anawadharau Waafrika wote. Fiona asema:

> "Fala kabisa wewe, twawezaje sisi kuwa ndugu wa tumbiri kama nyie?" (uk.27).

Katika ukurasa wa 29, Fiona na Bob walipokamilisha shughuli yao ya kumpora Fikirini, walimwacha na kumfukuza akiwa uchi. Kwa kawaida, mtu azaliwapo huwa uchi na hapa Fikirini analinganishwa na mtoto anapozaliwa kwa kuwa alikuwa amevuliwa nguo zote. Mwandishi asema:

> Fikirini hakusubiri aambiwe mara ya pili. Alijitosa nje, tupu tupu kama alivyozaliwa (Uk 29).

### 4.4 Gilasi ya Mwisho Makaburini

Hadithi hii inamuangazia sana mhusika mmoja – Msoi ambaye huoteshwa ndoto ambazo inasemekana mara nyingi hutokea kuwa za kweli. Ndoto hizi hunaswa kupitia ncha za malaika yake ambapo hisia hutua kwenye ncha hizo na kuingizwa bongoni ambamo tafsiri ya ndoto hutolewa. Inasemekana kuwa, mwezi mzima umepita tangu alipooteshwa ndoto ambayo haikuwa nzuri. Na kama kawaida, ncha za malaika ndizo zipokeazo ishara ya ndoto hizo. Mwandishi anaeleza jinsi ncha hizo za malaika ya Msoi zilivyosimama kama kijiti. Hii ni tashbiha iliyo na maana kuwa, ncha zilikuwa imara bila kupinda kama vile kijiti kinavyosimama. Mwandishi anasema:

> Mwezi mzima umepita baada ya ncha za malaika yake kusimama kama kijiti baada ya kunasa hisia fulani ya kitisho na wasiwasi (Uk 32).

Pia, mwandishi anaendelea kuonyesha jinsi hisia zinazopelekwa ubongoni zilivyokuwa zimevimba, tayari kupeleka ujumbe kwenye akili yake. Kuvimba huko kwa hisia kuna maana ya kutengenezeka kwa ndoto ambazo ishara yao tayari ilikuwa ishapokelewa na ncha za malaika.

Mwandishi anasema :

> Leo hisia hiyo kali ilikuwa imeumuka haraka kama hamuri lililojazwa hamira (uk32)

Kitendo cha kuumuka ni kule kufura kwa hamuri hasa linapotiwa kiungo kinachoitwa hamira. Hisia za Msoi zinalinganishwa na kufura kwa hamuri kwa jinsi ambavyo ziko tayari kusababisha ndoto.

Semkwa, rafikiye Msoi, aendapo nyumbani kwa Msoi ili kumbembeleza kwenda baa ya mavani, jambo ambalo Msoi alikuwa kinyume nalo kwa sababu ya ndoto mbaya aliyoiota kupahusu, anampata Msoi katepwereka juu ya sofa. Jambo hili linamshangaza Semkwa kwani haikuwa kawaida yake kutulia nyumbani wakati ambapo walipaswa kwenda kujipa burudani katika *Baa ya Makaburini.* Kulala kwa Msoi kochini kunafananishwa na kule kulala kwa mgonjwa wa Malaria. Semkwa analaumu:

> "He! Saa mbili na nusu sasa hujajitayarisha tu? Umebaki kulala kochini kama mgonjwa wa Malaria. Au ndiyo huendi?" (Uk 33).

Semkwa, anapoendelea kumshawishi Msoi kuandamana naye hadi baa yao ya makaburini, anatumia tashbiha nyingine kwa kulinganisha kulala chini kwa Msoi na kule kulala kwa mgonjwa wa homa aina ya Malaria. Kulinganisha huku huenda kukamshawishi Msoi kukubali rai ya Semkwa ya kuandamana naye. Semkwa anadai:

> Utabakije juu ya kochi kama mgonjwa wa homa na leo ni Jumamosi? (uk.33).

Katika mazungumzo ya marafiki hawa; Semkwa, Msoi, Josefina na Asha, watatu hawa wanamwingilia Msoi kuwa na msimamo mkali usiotetereka. Msoi anashikilia kuwa hawakufaa kuja kwenye baa hii kwani ndoto alizokuwa ameota hazikuashiria hali nzuri. Licha ya rafikize kumshawishi kuwa mambo yalikuwa shwari, Msoi anashikilia kuwa palikuwa na kasoro. Hali hii inapelekea Josefina kumlinganisha Msoi na Ziraili-- kiumbe kinachoaminika kuwa malaika wa kifo. Ziraili huaminika kusababisha mikosi. Msoi analinganishwa na Ziraili kwani ameshikilia kuwa kuna mkosi ambao ungetokea siku hiyo:

> "Bwana huyu akishikilia lake, aliongea Josefina ," kama Ziraili, mpaka aitoe roho ya kiumbe" (uk.35).

Walipokuwa wakibugia pombe, wote watatu walikunywa kwa kujistarehesha isipokuwa Msoi ambaye aliishia kunywa maji badala ya pombe. Jambo hili linawakera wenzake na wanajaribu kumlinganisha na mtoto ili kumdhihaki lakini Msoi anashikilia msimamo wake. Kwa kawaida, watoto huwa hawanywi pombe, na kwa kuwa Msoi amekataa kunywa pombe, basi analinganishwa na watoto. Asha anachokoza :

> "Hata maji unayasinzilia? Wewe utakunywa maji kama mtoto mpaka lini?" (uk36).

Asha anamuingilia sana Msoi licha ya Msoi kutokuwa na uchangamfu wa kawaida. Jambo hili linamkera Msoi licha ya urafiki wao na Msoi anamsuta Asha kwa kutumia tashbiha ifuatayo:

> "Na wewe sharti unigande mimi tu kama kupe?" (uk 36).

Msoi anamfananisha Asha na mdudu aitwaye kupe. Kupe anajulikana kwa kuwaganda binadamu na wanyama na kuwafyonza damu. Kupe akishaganda kwenye ngozi ya kiumbe ni muhali kumbandua. Asha naye anamwingilia sana Msoi pasi na kumpa muda wa kupumzika ndiposa Msoi anaudhika kidogo na kumfananisha Asha na kupe.

Marafiki hawa wanapoendelea kujipa burudani, mbali na vyakula na vingwaji, walijifurahisha pia kwa muziki. Katika kueleza minenguo na miondoko ya waliokuwa wakijifaragua, mwandishi anatumia tashbiha kuiweka wazi hali hii:

> Jozi mbilimbili. Minenguo, mikatiko, mibenuko, miondoko, mitetemeko kama wagonjwa wa Malaria, mitiririko ya jasho kama maji ya mlizamu wa mto. Furaha, furaha, furaha imechanua (uk37).

Hapa, pana mtindo wa kusakata rumba unaoshabihishwa na mitetemeko kama ya wagonjwa wa Malaria. Mtu auguapo ugonjwa wa Malaria hutetemeka sana na mtetemeko huu unafananishwa na mtindo mojawapo wa kucheza ngoma. Vile vile, kutokana na kucheza ngoma sana, watu walitokwa na jasho jingi sana. Hali hii ya kutokwa jasho inalinganishwa na jinsi maji ya mlizamu wa mto yatiririkavyo.

Katika hali hii ya kujiburudisha, Msoi na Asha wanashtukia kundi la vizuu kutoka mavani. Vizuu hawa walikuwa na sura na mwendo wa kutisha. Mwandishi anatumia tashbiha kuonyesha sura za nyuso zao kwa kusema:

> Kule mavani kundi la vizuu limejifufua kwa mtindo wa Thriller wa Michael Jackson. Linakuja kule baa kwa kujikongoja na kujitetemesha na kutoa sauti za kiufu. Nyuso nyeupe kama chokaa (uk37).

Nyuso za vizuu hawa zinafananishwa na chokaa. Chokaa ni rangi nyeupe inayotumiwa kupakia nyumba. Weupe wa nyuso unaonyesha jinsi viumbe hawa walivyokuwa wakitisha.

Katika ghasia zilizofuatia baada kuonekana kwa kundi la vizuu, kila mtu alijitafutia njia yake kujiokoa. Hata hivyo, kuna wengine ambao walilemewa na uoga na badala ya kutoroka walibaki kuzubaa. Mwandishi anawalinganisha hawa na masanamu. Sanamu ni kitu kilichochongwa aghalabu mfano wa kitu chenye uhai lakini chenyewe huwa hakina uhai. Mwandishi asema:

> Kuna walioshangaa na kukodoa macho na kung`ang`ana kama masanamu (uk 39).

## 4.5 Maeko

*Maeko* ni hadithi inayosimulia maisha ya ndoa kati ya Jamila na Hamduni na changamoto za ndoa hii zinazotokana na ulevi wa Hamduni. Mojawapo ya matatizo yanayomkumba Jamila ni kupigwa sana pindi mumewe awapo mlevi. Mwandishi anampambanua Duni kama aliyekuwa akimpiga mkewe pasi na kujali kuwa ni binadamu. Anasema:

> Duni alikuwa mpigaji mkubwa asiye mfano. Alimpiga mkewe kama ngoma ya kimanga popote apapatapo (uk53).

Jamila, anavyopigwa na mumewe analinganishwa na ngoma ya kimanga. Wamanga ni jamii inayojulikana kwa kupiga ngoma sana hadi kufikia kiwango cha kuipasua. Jamila anapofananishwa na ngoma ya kimanga inaonyesha jinsi anavyopigwa sana na mumewe.

Hata hivyo, licha ya ulevi wa Duni unaomsababisha kila mara kumpiga mkewe, anapolevuka yeye huwa tofauti kabisa. Mara nyingi huwa mwingi wa toba na majonzi mengi akiyajutia aliyoyafanya alipokuwa mlevi. Wakati huu, Duni alipolevuka alimhurumia sana mkewe kwa madhila aliyomsababishia. Jambo hili lilimliza sana Duni kiasi cha machozi yake kufananishwa na maji ya mvua kwenye ukingo wa bati. Hii ina maana kuwa, Duni alilia sana. Mwandishi anatumia tashbiha ifuatayo :

> Kufika hapo, Duni hakuweza kuyadhibiti tena machozi yake yaliyokwishavuka mipaka mashavu yake. Akayaacha yachirizike yapendavyo. Nayo yakachirizika mithili ya maji ya mvua katika ukingo wa bati (uk55).

Jamila anapopitia mateso katika ndoa yake, kunao watu mbalimbali wanaomshauri kwa njia mbalimbali kuhusu atakavyofanya kuyakwepa mateso ya mumewe. Wengine walimshauri akatae kuadhibiwa kama mwana asiye na kwao. Kulingana nao, kukubali kwa Jamila kuadhibiwa kunafananishwa na jinsi mtoto asiye na kwao awezavyo kuadhibiwa. Kwa hili, Jamila anashauriwa amuache mumewe iwapo ataendelea kumuadhibu maadamu ana kwao.

> Madhali na yeye mdomo na mikono anayo, akatae kuadhibiwa kama mwana asiye na kwao (uk53).

### 4.6 Kanda la Usufi

Hadithi hii inazungumzia mahusiano ya kimapenzi kati ya Sela na Masazu ambayo yanapelekea Sela kupata mimba akingali shuleni na kumletea masaibu chungu nzima. Mwandishi amefaulu pakubwa katika matumizi ya tashbiha. Mwanzoni, Sela na Masazu wakutanapo kwa mara ya kwanza, Masazu anaingiwa na msisimko wa namna yake. Kwa Masazu, fursa ya kuongea na msichana kama Sela si rahisi kupatikana. Mwandishi asema:

> Pindi Masazu alipomuona Sela, moyo ulimsisimka. Akajua nafasi kama hiyo hutokea kwa nadra ya jua kupatwa (uk.60).

Kupatwa kwa jua ni tukio la kimaumbile ambalo hutokea kwa bahati sana. Katika muktadha huu, Masazu kupata fursa ya kufahamiana na Sela ni kati ya nafasi adimu zaidi zinazoweza kutokea.

Pia, kutokana na kutokea kwa fursa kama hii, Masazu alijiandaa vilivyo ili aweze kunasa makini ya Sela. Tashbiha inayofuata inamfananisha Masazu na chui akiwa mawindoni. Naye Sela anafananishwa na windo la chui linaloingizwa mtegoni.

> Kama chui aliyelivizia windo lake na sasa limetokea akajiandaa (uk60).

Masazu anapojaribu kulinasa windo lake, anatumia uongo kuwa alikuwa akiumwa na kichwa ili Sela aweze kumsaidia. Masazu afikapo kliniki, Sela alimwelezea Sista kuhusu Masazu ambaye alikuwa akiumwa na kichwa. Mwandishi anasisitiza ujumbe wake kwa kueleza jinsi Masazu alivyojifanya kuhisi uchungu wa kuumwa na kichwa:

> ...alikuwa ameketi amekishikila kichwa kana kwamba kingedondoka (uk 60).

Sela kwa huruma, anampeleka Masazu kwenye kliniki ya shule ambapo alipewa vidonge vya kupunguza maumivu. Hata hivyo, Masazu hamezi vidonge vile na badala yake anavitema nyasini kama ambaye amevitapika. Kuona haya, Sela anakuwa na wasiwasi kuwa Masazu huenda akawa amezidiwa na ugonjwa na hivyo kumrai warudi katika kliniki. Hapa ndipo Masazu anapokataa katakata - mkatao unaofananishwa na ule wa mbuzi achomekaye kwato ardhini anapovutwa. Mbuzi ni mnyama mkaidi ambaye akikataa kutembea, hata umvute namna gani, huweza kuchomeka kwato zake ardhini na hivyo kumfanya vigumu kusonga. Katika hadithi hii, Masazu, kwa kuwa alifahamu kuwa ugonjwa wake haukuwa wa kweli, alikataa katakata kurudi kwenye kliniki. Masazu hapa analinganishwa na mbuzi anapokataa jambo:

> Akamsihhi warudi katika kliniki lakini Masazu akakataa katakata; mkatao wa mbuzi achomekaye kwato ardhini anapovutwa (uk.61).

Baada ya juma moja, Masazu alimwandikia Sela barua akimshukuru sana kwa utu wake. Sela alifurahia sana kwani hakuwa amepokea barua nyingine kutoka kwa mvulana yeyote. Alikuwa tu akiwasikia wanafunzi wenzake wakizungumzia barua walizotumiwa na marafiki zao wavulana wa shule nyingine. Kwa sababu hii, Sela aliitunza barua ile kama uhai. Katika tashbiha hii, barua inafananishwa na uhai kwa jinsi inavyochungwa. Kwa kawaida, uhai huchungwa sana hasa wa binadamu. Sela aliichunga barua ile kama mtu anavyoweza kuchunga maisha ya binadamu.

> Sasa alikuwa ameipokea barua iliyokuwa imepuliziwa marashi. Aliitunza barua ile kama uhai (uk61).

Mapenzi ya wawili hawa yaliendelea kunoga na walifanya mikutano ya faragha wakati wa likizo za shule na tamasha za muziki nafasi ilipojitokeza. Wakati mmoja Sela alitaka hakikisho kutoka kwa Masazu kuwa hangeyasaliti mapenzi yao. Masazu alimhakikishia Sela kwa kuapa kuwa mapenzi yao yalikuwa ya dhati na katu hangeweza kumsaliti. Kiapo hiki kinamuathiri pakubwa Sela na mwandishi anatumia tashbiha kueleza athari hii kwa Sela. Anasema:

> Kiapo hicho kiliyeyusha nafsi ya Sela. Kikalegeza kiwiliwili chake mithili ya mbwa anayekabiliana na chatu macho kwa macho. Mengine yalibaki katika himaya ya maumbile (uk61).

Kiapo hapa kinamfanya Sela afananishwe na mbwa ajilegezapo anapokabiliana na chatu. Chatu ni joka lililo na uwezo na nguvu nyingi kuliko mbwa. Kwa sababu hii, mbwa akabilianapo na chatu hujua fika kwamba atazidiwa nguvu. Sela anapolinganishwa na mbwa ina maana kuwa nguvu zilimwishia na hivyo kumpa fursa Masazu (chatu) aliye na nguvu kutawala. Hii inaonyesha jinsi wasichana wanavyoathirika na mapenzi kwa urahisi.

Kadiri muda ulivyosonga inambainikia Sela kuwa yu mjamzito. Sela alidhurika sana kutokana na hali yake. Alikosa utulivu masomoni na hakujua maisha yake yangechukua mkondo upi. Ndiposa mwandishi anamlinganisha Sela na tiara - kifaa kinachopeperushwa na upepo, pasi na kujua kitakapotua.

> Ulimwengu wake ulivurugika, akawa kama tiara inayopeperushwa na upepo ikaenda arijojo (uk61).

Kufikia mwishoni mwa hadithi, Masazu na Sela walishaanza kuishi pamoja kama mke na mume. Hata hivyo, hawakuruhusiwa kukichukua kitoto chao kidogo kwani hawangemudu utaratibu wa kawaida wa kuenda kwa wazazi wa Sela kwa sababu ya uchochole. Kwa hivyo, walipanga njama ya kumwiba mtoto nyakati za usiku kwa usaidizi wa dadake Sela, Rozina aliyekuwa akimlea mtoto.

Usiku wa manane, Sela na Masazu walimwamsha kwa utaratibu Rozina ili wasije wakagunduliwa. Rozina aliamka na kuwakabidhi Sela na Masazu mtoto wao. Rozina alifanya hivyo kwa makini sana ili mtoto asije akaamka na siri yao kugunduliwa. Mwandishi hapa anamfananisha Rozina na rubani wa ndege jinsi anavyokuwa makini aendeshapo ndege.

> Kadogo alikuwa kalala fofofo. Rozina alimchukua vivyo hivyo na kumpitisha taratibu na kwa makini dirishani kumkabidhi baba yake. Alifanya hivyo kwa makini ya rubani wa ndege. Maana kuamka kwake na kilio ambacho bila shaka kingefuatia kingewaborongea mkakati (uk.64).

## 4.7 Tazamana na Mauti

Hadithi hii inasimulia maisha ya msichana – Lucy anayetaka kwa vyovyote vile kuishi Uingereza na hasa mji wa London. Tamaa ya Lucy ya kuenda kuishi London inafananishwa na kiu ya mtu asafiriye jangwani kwa muda mrefu bila maji. Jangwani ni mahali pakavu na huchochea kiu hasa kwa binadamu kwa sababu ya kupoteza maji mengi mwilini. Hamu ya maji jangwani aghalabu ni vigumu kuituliza kwa kuwa maji hayapatikani jangwani. Mwandishi anamlinganisha Lucy na tamaa yake ya kuishi London kama mtu asafiriye jangwani:

> Basi siku zote hizo kiu ya kwenda kuishi London ilikuja kumkaa mioni, ikamchagiza kama vile kiu ya mtu aliyekuwa akisafiri jangwani kwa miaka bila ya kuyagundua maji (uk 91).

Lucy anapozidi kutafuta mbinu mbalimbali za kufika London anaibua wazo la kuolewa na mwanamume kutoka Uingereza ili waende naye huko. Lakini swala kuu linalombabaisha ni; huyu mwanamume kutoka Uingereza atayekuja kumuoa yeye yuko wapi? Anajipa moyo kwamba ana kila kinachohitajika na mwanamume kama vile sura ya kupendeza na hali kwamba bado angali kijana. Mwandishi anampamba Lucy kwa kutumia tashbiha ifuatayo;

> Sura ya kuvutia anayo, akivaa anapendeza. Damu ya ujana inamchemka. Joto la mwili wake linaweza kuwa kama kiota cha ndege kwa mwanamume yeyote mwenye baridi (uk92).

Hapa, joto la mwili wa Lucy linafananishwa na kiota cha ndege. Kiota ni mahali patulivu ambapo ndege hujipumzisha na kujipumbaza baada ya shughuli za mchana kutwa.

Lucy anapolinganishwa na kiota ina maana kwamba uzuri wake unaweza kumvutia na kumhifadhi mwanamume asiweze kifikiria kutoka. Naye mwanamume anayetazamiwa na Lucy analinganishwa na ndege ambaye hurudi kiotani palipo na utulivu na starehe.

Hata hivyo, mbinu ya Lucy ya kufika Uingereza kupitia kuolewa inakumbwa na changamoto si haba. Mara nyingi Lucy hupitapita jijini ili aonekane na Wazungu na anapokumbana nao yeye huwapa tabasamu na wao humtabasamia tu na kupita na shughuli zao kinyume na matarajio ya Lucy na fikira nyingi na majuto moyoni. Mwandishi asema;

> Wengi walitabasamu naye siku zote hizi, lakini wakishafanya hivyo humpita kama upepo wa kimbunga na kumwacha yeye mgonjwa wa tamaa (uk92).

Mpito wa Wazungu hawa unalinganishwa moja kwa moja na upepo mkali – kimbunga, kinavyopita na kisionekane tena. Hii inaashiria hali ambapo Wazungu wampitapo Lucy, huwa hana matumaini tena ya kuwafikia Wazungu hawa. Baadaye, Lucy hafi moyo na anaamua wakati huu kwenda kuingia sinema baada ya kuchoka siku nzima. Pale kwenye sinema, anakumbana na babu wa Kizungu ambaye pia yeye alikuwa akitaka kuingia kwenye sinema. Kwa bahati nzuri, Lucy anamwona mzee yule akipepesuka karibu kuanguka. Kabla hajaanguka, Lucy anamfikia kwa haraka na kumsaidia ili asianguke na kuumia. Jinsi Lucy alivyomkimbilia kumwokoa mzee yule ndivyo mwandishi anavyosimulia kwa kutumia tashbiha kuwa Lucy alikuwa kama mshale. Lucy hapa anafananishwa na mshale kwa jinsi alivyofyatuka mbio kumwokoa mzee Yule asianguke chini.

> Lucy aliruka kama mshale, akamwahi kwa nukta ya dakika kabla ya kufika chini na kugonga kichwa chake sakafuni na kuwa sababu ya mauti yake (uk94).

**4.8 Hitimisho**

Katika sura ya nne, tumeshughulikia mbinu ya tashbiha kama ilivyotumiwa na waandishi wa hadithi teule za diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* kuwasilisha dhamira mbalimbali. Imebainika kuwa, nyingi za hadithi tulizoziteua zimetumia mbinu hii kwa ufaafu. Hata hivyo, hadithi *Kikaza* haijadhihirisha matumizi yoyote ya mbinu hii. Katika sura itakayofuata, tumeshughulikia matumizi ya taashira katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.*

## SURA YA TANO

## 5.0 Matumizi ya Taashira katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

### 5.1 Utangulizi

Taashira, kama tulivyoeleza katika sura ya pili, ni matumizi ya lugha ya ishara kuwakilisha ujumbe fulani ambapo jina au kitu fulani kinatumika kumaanisha kitu kingine chenye uhusiano na kile kilichotumiwa. Katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi nyingine,* waandishi wametumia lugha ya ishara pakubwa ili kuangazia maswala mbalimbali katika hadithi zao. Katika kushughulikia matumizi ya taashira katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, tutajikita katika hadithi saba zifuatazo:

### 5.2 Samaki wa Nchi za Joto

Anwani *Samaki wa Nchi za Joto* ni taashira. Samaki hawa wametumiwa kumaanisha kitu kingine mbali na kinachofahamika kikawaida kama samaki. Ishara ya kwanza ya samaki hawa ni biashara iliyonoga inayofanywa na Peter ambapo hununua samaki kwa bei rahisi kutoka nchi za Afrika na kuwauza ng`ambo kwa bei ghali mno. Taashira hii inaonyesha dhuluma za kiuchumi dhidi ya Waafrika. Pia, nchi za jotó ni taashira inayoashiria nchi za Afrika ambako ukandamizaji unaendelezwa na Wazungu licha ya mataifa ya Afrika kupata uhuru. Naye Peter, jina la Kiingereza, ni ishara ya nguvu na mamlaka katika nyanja aghalabu zote za kimaisha mathalan; kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Isitoshe, *Samaki wa Nchi za Joto* huenda ikawa na maana ya wasichana wa Kiafrika wanaodhulumiwa kimapenzi na Wazungu. Mathalan, Christine, ambaye ni msichana wa Kiafrika anayesomea chuo kikuu anatumiwa na Mzungu, Peter, kukidhi haja zake za uchu wa kimapenzi bila kuwa na nia ya kumuoa baadaye.

Pia, sangara ni aina ya samaki wakubwa ambao wanaashiria wakoloni. Sangara hawa wanasemekana kuwala samaki wadogo waliokuwa adimu kupatikana ulimwenguni na waliopatikana katika maeneo ya nchi za joto pekee.

Samaki wadogo walioliwa na sangara ni Waafrika na jinsi walivyodhulumiwa na Wazungu kwa kunyang'anywa mali yao ya kuwaendeleza kiuchumi.

Christine anapojiingiza kwenye uhusiano wa kimapenzi na Peter, anatahadharishwa na rafikize na hata dadake dhidi ya uhusiano huo. Peter anajulikana kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wasichana wengine mbali na Christine. Wikendi moja, Zac, rafikiye Christine, alimweleza Christine kuwa Peter alikuwa ameandamana na msichana mwingine huko *Entebbe Sailing Club*. Kusikia haya, Christine hakuwa na shughuli ya yale aliyoelezwa. Kwa kawaida, msichana hangependa kuwa na mwanamume mwenye mahusiano na wasichana wengine. Mambo hapa ni kinyume. Christine anatumia neno 'kitumbua' kuashiria uhusiano wake na Peter, na ambacho hakutaka kukitia mchanga au kusitisha uhusiano huo.

> Sikutaka kukitia kitumbua cha uhusiano wetu na Peter mchanga (uk16).

Isitoshe, Christine anajiona kuwa wa thamani kubwa kwa sababu amesoma sana na atakuwa na shahada. Anapowazia suala la ndoa, anapania kuolewa katika familia ya kitajiri kwa sababu thamani yake inatosha kumpata mume tajiri. Hapa, Christine anajiita Jersey au Fresian, ambao ni ng`ombe wa Kizungu wanaotoa maziwa mengi na hivyo thamani yao ni ya juu .Hataki kujilinganisha na ng`ombe wa kienyeji wa Ankole wasio na thamani. Friesian na Jersey ni ishara ya vitu /watu wenye thamani ya juu ilhali Ankole ni ishara ya watu walio na hadhi ya chini. Christine asema;

> Kuolewa kulikuwa afadhali, kuolewa katika familia ya kitajiri. Nikiwa na shahada ningekuwa kama ng`ombe wa Kizungu. Niliwaza Friesian au Jersey sio wale wa Ankole wenye pembe zilizojiotea ovyo (uk17).

Ama kwa kweli, mbinu ya taashira imetumiwa kwa wingi katika diwani hii ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* kama inavyoonekana hapa chini katika hadithi ya *Damu Nyeusi* iliyo katika mkusanyiko huu wa hadithi.

## 5.3 Damu Nyeusi

Katika hadithi hii, mwandishi ametumia mbinu ya taashira kuwasilisha dhamira. Mathalan, anwani *Damu Nyeusi* ni taashira inayomaanisha Waafrika. Kwa kawaida, damu huwa nyekundu lakini inapoitwa nyeusi ina maana ya Uafrika. Kitu cheusi kwa kawaida kinaashira giza au kutokuwepo kwa mwangaza. Marekani, kulingana na hadithi hii, Waafrika wanaonekana watu duni, wasiostaarabika na walio nyuma kimaendeleo. Ndiposa pale Marekani, Fikirini anadhulumiwa pakubwa kwa sababu ya rangi yake nyeusi.

Licha ya rangi nyeusi kuashiria mtu Mwafrika, weusi pia unatoa ishara ya kudhalilishwa kwa mtu mweusi (Mwafrika). Aghalabu matendo yote maovu yananasibishwa na watu weusi. Fikirini anachelewa kufika chuoni kwani basi lililokuwa likiendeshwa na Mzungu limemwacha kwa kuwa ni Mwafrika. Inasemekana kuwa dereva huyo alifikiria kuwa Fikirini ni jambazi kwa kuwa ni mweusi. Fiona anathibitisha haya anapomwambia Fikirini:

> "Ahaa! Alikuwa Dereva Mzungu alipokuona akafikiria wewe ni jambazi?"
> "Ananiona mimi ni jambazi kwa sababu mimi ni mweusi" (uk26).

Katika kuelezea mazingira ya Marekani, mwandishi anatumia taashira 'weupe'. Weupe huu ni wa watu na wa mazingira. Wengi wa watu wa Marekani ngozi zao ni nyeupe. Aidha, mazingira yao yanatajwa kuwa meupe kwa sababu ya theluji iliyoyafunika. Weupe huu ni ishara ya nguvu au mamlaka. Ndiposa mwandishi analamika akisema;

> Weupe…kila kitu cheupe katika nchi hii, mtu mweusi apate wapi sauti na satua? (uk22).

Isitoshe, tumbiri ni ishara ya udhalilishaji wa Waafrika. Kwanza, wanafunzi pale chuoni wanamuuliza Fikirini maswali ya kumwudhi kwamba ikiwa kwao Afrika wao huishi kwenye miti kama tumbiri. Isitoshe, Fiona anayathibitisha haya kwa kumwita Fikirini tumbiri. Kwa kawaida, tumbiri ni mnyama lakini katika muktadha wa hadithi hii, neno tumbiri limetumika kitaashira kumdhalilisha mtu mweusi (Mwafrika).

Zaidi ya hayo, hadithini mna taashira ya taa za rangi nyekundu ambazo huashiria kuwa watu wasivuke barabara. Mwako huu wa taa nyekundu ndio unaopelekea Fikirini kushtakiwa na kutozwa faini avukapo barabara ilhali Wazungu hawachukuliwi hatua yoyote. Hebu tuangalie matumizi ya taashira katika hadithi ya *Gilasi ya Mwisho Makaburini* na ambayo vilevile hupatikana katika mkusanyiko wa hadithi za *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.*

**5.4 Gilasi ya Mwisho Makaburini**

Hii ni hadithi iliyojaa lugha ya taashira. Ndoto za Msoi hutoa ishara ambazo kwa kiwango kikubwa ni za kuaminika. Mambo anayoyaota hutokea. Mathalan, alipoota kuwa pangetokea jambo baya katika *Baa ya Makaburini,* mwishowe ndoto hiyo ilitimia.

Pili, makaburini ni ishara ya utulivu. Utulivu huu unatokana na sababu kwamba "waishio" makaburini ni wafu ambao kwa kawaida huwa hawana zogo. *Baa ya Makaburini* ni tulivu na hii ndiyo sababu kina Msoi na rafikize hupapendelea. Baa ni mahali pa kujistarehesha na panahitaji utulivu. Kwa baa hii kuwekwa makaburini, ni ishara ya kuonyesha utulivu upatikanao huko.

Aidha, imani ya kishirikina ya Msoi inamfanya kuona kulia kwa ndege mbaya kuashiria jambo baya. Mwandishi asema;

> Ana wasiwasi ndiyo, lakini hajui wasiwasi huo wa nini. Anaona kuna kitu kinacholizia ndege mbaya, lakini hajui kitu gani wala hajui ndege huyu ana sura na kusudi gani (uk.33).

Isitoshe, kulingana na Msoi, radi iliyopiga wakati Msoi na Semkwa walipokuwa njiani kuelekea *Baa ya Makaburini* haikuwa ya kawaida. Kwa Msoi, radi ni ishara ya jambo baya. Mwandsihi asema;

> Kwa Msoi hiyo ilikuwa ishara mbaya, lakini hakutaka kusema lolote asije akaambiwa yeye ni mshirikina. Semkwa aliona radi ni jambo la kawaida, jambo la kimaumbile tu (uk34).

Vilevile, majambazi waliovamia baa ya makaburini wanajitokeza kama vizuu, ishara kwamba wafu walikuwa wamefufuka kutoka makaburini. Inasemekana kuwa kundi hilo la vizuu lilikuja kule kwa baa kwa kujikongoja na kujitetemesha na kutoa sauti za kiufu. Taashira ya vizuu ilidhamiria kuwaogofya wateja katika baa ya makaburini ili kuwapora. Isitoshe, tone moja la chozi katika ukurasa wa 34 lina ishara ya mvua, kwamba haikunyesha hata kidogo .

> Mbingu ilifanya hivyo mara moja tu. Tena bila ya kutiririsha hata tone moja la chozi (uk34).

Zaidi ya hayo, anwani *Gilasi ya Mwisho Makaburini* ni ya kitaashira. Katika muktadha wa baa, gilasi ni chombo kitumiwacho kunywea vileo. Glasi hii inaashiria unywaji wa pombe kule kwenye *Baa ya Makaburini*. Burudani hii, kwa kunywa pombe, yasemekana kuwa ndiyo ya mwisho kwani baada ya kisa kilichowakumba masahibu hawa, inakisiwa kwamba hawangethubutu kurudi kule tena. Kwa hivyo, anwani ni taashira iliyo na maana kuwa huu ndio uliokuwa mwsiho wa starehe za jamaa hawa katika baa ile ya mavani. Yafuatayo ni matumizi ya taashira katika hadithi ya *Kikaza.*

### 5.5 Kikaza

Hii ni hadithi iliyosheheni taashira si haba. Kwanza, anwani "*Kikaza*" ni taashira ya uongozi. Hii ndio maana inasemekana kuwa ushonaji wa kikaza ulikuwa jukumu la umma mzima ikimaanisha kwamba raia walikuwa na jukumu la kuteua viongozi wao. Vilevile, mwanzoni mwa hadithi panaonekana mawingu mazito meusi (uk41). Hii ilikuwa ishara ya mvua kama inavyofahamika kuwa dalili ya mvua ni mawingu au hali mbaya ya kisiasa. Aidha, kulitokea jambo lisilokuwa la kawaida ambapo giza siku hizo lilianza kuingia saa tisa mchana. Hii ilikuwa ni ishara ya hali ya kijijini kuwa ya kutatanisha au kutotabirika. Katika mataifa mengi ulimwenguni, kutokeapo mchafukoge wa kisiasa, kafu huwekwa ambapo wakati wa watu kutoka nje hubanwa. Mawingu mazito vilevile yanaweza kuashiria kafu.

Pia, mingurumo ya radi inayoshuhudiwa katika ukurasa wa 41, ni taashira ya utabiri wa kuporomoka kwa uongozi wa Bwana Mtajika. Isitoshe, kuna kisa cha kuanguka kwa kobe ambacho pia kinaashiria kuporomoka kwa uongozi wa Bwana Mtajika. Kabla ya hili, kobe anaonekana kupaa, ishara kwamba Bwana Mtajika alikuwa kwenye uongozi lakini hatimaye akaja kuanguka wakati ambapo uongozi wake uliisha. Hatimaye, kuna kunyesha kwa mvua ambako kunaashiria mabadiliko au suluhisho la matatizo ya wanakijiji (uk 48). Mvua siku zote huwa ni ishara ya neema na mema na ndio maana tunasema kuwa kunyesha kwake kunaashiria kupatikana kwa suluhisho la matatizo ya wanakijiji. Licha ya hayo, upepo unaovuma wakati wanakijiji wanapoenda ikuluni ni ishara ya matarajio ya kumngo`a Mtajika mamlakani (Mapinduzi ).

Zaidi ya hayo, kupasuka kwa kikaza ni ishara ya kuporomoka/kutofanikwa kwa uongozi wa Mtajika. Katika jamii nyingi ulimwenguni, viongozi huwa na vitu vinavyoashiria uongozi. Katika muktadha wa hadithi hii, tunapata kuwa ni kikaza. Kwa hivyo, kinapopasuka, hii ni ishara tosha kuwa uongozi wa Mtajika umefikia kikomo.

### 5.6 Maeko

Hadithi hii, japo kwa uchache, imetumia mbinu ya taashira. Kwanza, anwani ya hadithi *"Maeko"* ni ya kitaashira. Anwani hii ina maana kuwa, kuna mambo yanayomfanya Jamila kusalia katika ndoa ile licha ya mateso kutoka kwa mumewe. Mambo yamwekayo Jamila ndiyo yanayoitwa maeko. Baadhi ya mambo haya ni kama vile, kupikiwa chakula na mumewe na kufuliwa nguo, mambo ambayo wengine hawayapati kutoka kwa waume zao.

Pili, Firauni katika hadithi hii ni ishara ya mateso waliyoyapitia Wanaisraeli chini ya uongozi wa Wamisri. Hapa, mateso haya yanaendelezwa na Duni dhidi ya mkewe, Jamila. Aidha, Jamila aitwapo kinda ni ishara ya kuwa na thamani kubwa hata kulindwa kama ndege mchanga. Washauri wa Jamila wanashangaa namna Jamila, licha ya udogo wa umri na astahiliye kulindwa, anavyoteswa na mumewe.

Haitarajiwi mke wa umri mdogo kama Jamila kupitia mateso anayoyapitia kutoka kwa mume wake. Hatimaye, ulimwengu umeelezwa kwa kutumia taashira – Sayari ya Mungu. Wanaomhurumia Jamila wanashangazwa na kinachomfanya Jamila kuvumilia mateso kutoka kwa Duni kana kwamba ndiye aliyekuwa mwanamume pekee katika dunia. Mwandishi anadhihirisha hili kwa kuuliza:

> Kwani Duni alikuwa mwanamume pekee katika sayari hii ya Mungu? (uk.51).

**5.7 Kanda la Usufi**

Hadithi hii inahusu mapenzi kati ya Sela na Masazu ambao ni wanafunzi wa shule ya upili. Masazu anapotaka kumhakikishia Sela kuwa alikuwa na mapenzi ya dhati kwake, anagusisha kidole chake ardhini kisha anakiramba. Hii ni ishara ya kiapo kuwa hangeweza kumsaliti mpenziwe na iwapo ingetokea hivyo, basi alikuwa radhi kufa (mchanga). Mchanga ni ishara ya mauti na ufu kwa kuwa katika tamaduni nyingi, watu wafapo huweza kuzikwa mchangani.

Pili, nguo za mararu zinazovishwa mtoto wa Sela na Masazu ni ishara ya umaskini uliowagubika. Kwa kuwa walikuwa wangali shuleni, Sela na Masazu hawakuweza kumudu gharama ya kumnunulia mwana wao mavazi mazuri. Hali hii inakwenda kinyume na kaida ambapo mtoto anapozaliwa huvishwa nguo mpya na hata kupewa zawadi chungu nzima.

Isitoshe, umeme na radi ulioandamana na mvua kali ni ishara ya hofu na hatari iliyowangoja waja hawa walipokuwa katika safari ya usiku ule. Mwanga mkali (umeme) na sauti za ngurumo (radi) ni ishara ya kuogofya. Safari ya usiku ni ishara ya Sela na Masazu kutokujua kule waendako maishani.

Zaidi ya hayo, msiba unaozungumziwa katika ukurasa wa 63 na mamake Sela ni ishara ya shida. Mamake Sela anamkumbusha mumewe – Mzee Butali kuwa maadamu Sela ni mjamzito na ni mwana wao, basi jukumu la kukubali makosa lilikuwa lao wote. Jukumu linakuwa lao wote kama ishara ya kufeli kwao katika jukumu lao la kimsingi la malezi. Lau kama wangemlea mtoto wao kwa misingi miema, huu ujauzito usingepatikana sasa bali baadaye baada ya kumaliza masomo.

### 5.8 Tazamana na Mauti

Katika hadithi hii, mhusika mkuu Lucy ana ndoto ya kuishi London.*Ndoto* limetumika kitaashira kumaanisha azma aliyo nayo Lucy ya kuishi London. Baadaye, tunaona kuwa ndoto yake Lucy inatimia na anahamia London.

Pia, maji kwa kawaida ni kinywaji kinachonywewa ili kutuliza kiu. Kiu ni hamu ya kunywa maji. Hapa, Lucy alikuwa na kiu kubwa ya kuenda kuishi London. Kiu hii inamzidi na anajiuliza iwapo atawahi yagundua maji. Maji, katika muktadha huu ni kutimia kwa ndoto ya kutulizwa kwa tamaa ya Lucy ya kuishi London. Mwandishi asema;

> Basi siku zote hizo kiu ya kuenda kuishi London ilikuja kumkaa mioni, ikamchagiza kama vile kiu ya mtu aliyekuwa akisafiri jangwani kwa miaka bila kuyagundua maji. Lini atayaona maji? Alijiuliza (uk91).

Aidha, kuna taashira ya minyororo ambayo kulingana na mwandishi ni vikwazo, ambavyo vinamfunga Lucy kukosa fursa ya kwenda Uingereza. Lucy ana imani kuwa atavunja minyororo hii yote na kuafikia lengo lake la kuishi London. Kwa mfano, Lucy anakumbana na vikwazo kama kupitwa na Wazungu kama kimbunga pindi tu wamsalimiapo. Pia, Lucy anajaribu kutathmini njia kadhaa zitakazomwezesha kuishi London lakini njia zote hizi zina kasoro.

Zaidi ya hayo, Lucy anapokwenda sinema, anashuhudia kisa cha mwanamke wa Kiafrika na mwanamume wa Kizungu ambapo wanapeperushwa na upepo mkali wa dhoruba hewani. Yule mwanamke hatimaye alianguka chini akavurugikavurugika, lakini yule mwanamume alizidi kupeperushwa na upepo hadi akatokomea. Hii ni ishara ya mambo yaliyomkumba Lucy mwishoni mwa hadithi kwani alifariki na kumwacha mzee Crusoe akiendelea kuugua.

### 5.9 Hitimisho

Katika sura ya tano, tumeshughulikia mbinu ya taashira na jinsi mbinu hii ilivyojitokeza katika hadithi saba tulizoziteua kwa ajili ya utafiti. Aina zote tatu za taashira zimetumiwa na waandishi wa hadithi hizi kwa ufaafu na ufanisi mkubwa lakini sinekidoki na taniaba ndizo aina za taashira zilizotamalaki kwenye hadithi tulizokuwa tukizishughulikia. Mchango wa tamathali hii ya usemi umeleta tasfida na vilevile kufanya masimulizi kunoga kwa mnato wa lugha ilivyotumika.

## SURA YA SITA

## 6.0 Muhtasari, Mahitimisho na Mapendekezo

### 6.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia hitimisho la utafiti wetu na kuthibitisha maswali yetu ya utafiti na hatimaye tumetoa mapendekezo yetu kwa watafiti wa baadaye.

### 6.2 Muhtasari

Katika sura hii, tumetoa muhtasari wa masuala yaliyoshughulikiwa katika utafiti wetu mbali na mahitimisho na mapendekezo. Katika tasnifu hii, tumechunguza jinsi tashbiha, istiari na taashira zilivyotumiwa na waandishi wa hadithi zilizomo katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* na jinsi mbinu hizi zilivyochangia katika kuwasilisha dhamira na maudhui ya waandishi hawa.

Kazi hii imetoa ufafanuzi wa mihimili ya nadharia ya elimumitindo kwa kuihusisha na tashbiha, istiari na taashira. Tamathali hizi zimetolewa ufafanuzi wa kina na kuainishwa na kutolewa mifano mwafaka. Aidha, tumeonyesha uhusiano uliopo kati ya tamathali hizi za usemi kwani zote hurejelea dhana moja—ulinganisho wa sifa za kilinganishi na kilinganishwa.

Vilevile, katika utafiti huu, tumeangazia matumizi ya istiari na jinsi ilivyotumiwa kuwasilisha dhamira katika hadithi teule za diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Tumeonyesha jinsi istiari hizi zinavyoweza kuainishwa kwa misingi ya vilinganishi vyake mbalimbali.

Mbali na kufanya hili, tumehakiki matumizi ya tashbiha na jinsi zilivyochangia uwasilishaji wa dhamira katika hadithi tulizoziteua. Utafiti wetu umethibitisha kuwa tashbiha zinazojitokeza katika hadithi nyingi zimeainishwa kwa misingi ya vilinganishi vyake.

Halafu katika kuhitimisha, kazi hii imeshughulikia jinsi mbinu ya taashira ilivyotumiwa kuendeleza dhamira na maudhui katika hadithi tulizoziteua. Taashira za aina mbalimbali zimetumiwa kurejelea viumbe na hali mbalimbali. Kutokana na tamathali hizi za usemi, hadithi zilizomo katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* zimedhihirisha mnato wa aina yake na ufundi wa hali ya juu wa waandishi ambapo wameweza kufafanua dhana na hali mbalimbali za kawaida kwa kutumia lugha kwa ustadi ili kuweza kufikia hadhira lengwa.

## 6.3 Mahitimisho

Utafiti huu umeonyesha mbinu za tashbiha, istiari na taashira katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Tumezionyesha mbinu hizi katika sura ya tatu, nne na tano ambapo tumefafanua matumizi ya tamathali hizi kama zilivyojitokeza katika hadithi zilizoteuliwa. Aidha, tulitathmini mchango wa tamathali hizi za usemi katika kuwasilisha dhamira katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Hili limeshughulikiwa katika sura hizo za awali ambapo kila mbinu imeonyeshwa ilivyojitokeza katika hadithi mbalimbali.

Dhima ya tamathali hizi za usemi imejitokeza kwa namna mbalimbali. Kwanza, tamathali hizi zimetumika kufupisha maelezo kwa kuchora picha fulani akilini mwa msomaji. Picha hiyo ni ulinganisho wa kilinganishi na kilinganishwa. Pili, tamathali hizi zimetumika kufafanua maana ya vitu na dhana mbalimbali. Hali hii imepelekea kuboresha kazi ya mwandishi kwa ujumla kwa kuongeza ujumi wa kisanaa. Tatu, tumethibitisha kuwa tamathali hizi zimeweza kutoa ujumbe kwa njia fiche na hivyo kuleta tasfida.

Kwa kuzingatia maswali ya utafiti, tumethibitisha kuwa waandishi wa hadithi teule za *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* wametumia mbinu za tashbiha, istiari na taashira katika uandishi wao. Pia, makisio yetu kuwa tamathali hizi za usemi zimetumika kwa ufaafu kuwasilisha dhamira katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* ni ya ukweli.

## 6.5 Mapendekezo

Katika utafiti wetu, tumejikita katika kipengele mojawapo cha mtindo ambacho ni lugha. Tunatoa pendekezo kuwa, wahakiki wengine washughulikie vipengele vingine vya mtindo kama vile wahusika, usimulizi na mandhari katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi nyingine*. Pia, nadharia tuliyoitumia katika uchanganuzi wetu ni ya uhakiki wa kimtindo. Tunapendekeza kuwa wahakiki wengine wachambue hadithi hizi kwa kuzingatia nadharia nyingine kama vile ya umuundo, uhalisia na nyinginezo.

Isitoshe, kwa kuzingatia upeo na mipaka ya utafiti wetu, tumeangazia hadithi saba kati ya hadithi kumi na tatu zilizomo katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Tunatoa pendekezo kuwa wahakiki wa baadaye washughulikie hadithi nyingine zilizosalia kwa kuangazia tamathali za usemi tulizoziangazia. Aidha, tamathali za usemi ni nyingi lakini tuliteua tatu tu. Tunapendekeza kuwa watafiti wa baadaye washughulikie tamathali nyingine za usemi kama vile chuku, balagha na uhuishi.

## MAREJELEO


Barry, P. (2002) *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory. 2nd Edition.* Manchester University Press. U.S.A.

Chapmann, R. (1973) *Linguistics and Literature: An Introduction to Literary Stylistics.* London. Edward Arnold.

Crystal, D. na Davy, D. (1969) *Investigating English Style*. London: Longman Group.

Indagasi, H. (1988) *Stylistics.* Nairobi. Nairobi University Press.

Karanja, M.W. (2014) '*Matumizi ya Istiari, Tashbiha na Taashira katika Diwani ya Sauti ya Dhiki'.* Tasnifu ya Uzamili. Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kibera, V.(mh.) (1988) *An Anthology of East African Short Stories.* Harlow: Longman Group LTD.

Kineene wa Mutiso (2005) *Utenzi wa Hamziyya.* Dar es Salaam.TUKI.

Kuhenga, C. (1977) *Tamathali za Semi.* Dar es Salaam. E.A.L.B.

Kitsao, J. (1975) "*A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts".* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Leech, G.M. (1969) *A Linguistic Guide to English Poetry.* England. Longman.

Leech, G.M. na Short, M.(1981) *Style in Fiction: An Introduction to English Fictional Prose*. London. Longman.

Lugwiri, P.L. (2011) *'Sitiari, Taashira na Tashbiha katika Uwasilishaji wa Dhamira katika Utenzi wa Tambuka.'* Tasnifu ya uzamili. Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mbatiah, M. (mh.) (2000) *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Mbatiah,M. (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi. Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mbuthia, E. (2005) *"A Stylistic and Thematic Analysis of Kiswahili Short Stories".* Tasnifu ya Uzamifu. Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mohamed, S.A. (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi*. Nairobi. East African Educational Publishers.

Mohochi, E. (1995) *'Fani katika Hadithi Fupi za Kiswahili'*. Tasnifu ya Uzamili. Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Egerton.

Msokile, M. (1992) *Misingi ya Hadithi Fupi* .Dar es salaam University Press.

Msokile, M. (1993) *Msingi wa Uhakiki wa Kifasihi* . Dar es salaam East African Educational Publishers.

Murumba, J.B. (2013) '*Mtindo katika Watu wa Gehenna*'. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwanzi, H. (1995) "*The Style of The Short Story in Kenya: An Analysis of the Short Stories of Ngugi wa Thiong'o, Leonard Kibera and Grace Ogot".* Tasnifu ya uzamifu. Haijachapishwa. Chuo kikuu cha Nairobi.

Ngara, E. (1982) *Stylistic Criticism and the African Novel.* London. Heinemann.

Njogu, K. naChimera, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Olali, T. (2010) *Structure and Anti-Structure of Swahili Novel. A Stylistic Analysis of 'Babu* Alipofufuka' The Nairobi Journal of Literature no.6.

Senkoro, F.E.M.K. (1982) *Fasihi.* Dar es Salaam. Press and Publicity Centre.

Simpson, P. (2004) *Stylistic: A Resource Book for Students*. London. Routledge.

Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. JKF.

Wales, K. (2001) *A Dictionary of Stylistics. (2nd Edition*) England. Pearson Education LTD.

Walibora, K. na Mohamed, S.A. (2007) *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Nairobi. Moran Publishers.

Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Publishers.

Wamitila, K.W. (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Vide-muwa Publishers. Nairobi.